Haliuzwi

SEPTEMBA 7, 2026

/islamicftz

Rabi ul-Awwal 25 1448

# IMAAN

ISSN 5618 - NO. 600


Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah



## PM akataa misururu mirefu kusindikiza viongozi"

# Sheikh Bane ausia wanawake wa Kiislamu: Jitambueni, jithamininini





Soko la halal linavyovuka mipaka ya chakula na nyama

TPA, DP World zaweka rekodi mpya Bandari ya Dar

## Mzee Ameir: Maisha ya utulivu, aondoka, akiacha alama zake

- Aref Nahdi (Mwenyekiti, The Islamic Foundation), Viongozi Afrika wamfariji Rais Samia









Mzee Hafidh Ameir Hassan, aliyekuwa mume wa Rais Samia Suluhu Hassan, alizikwa katika shughuli ya maziko iliyofanyika Kizimkazi mjini Unguja

## KUTOKA MIMBARI ZETU

### MASJID AL-HARAM

Imam wa Makka ataja funguo za riziki yenye baraka kwa waumini



### MASJID HAQQ

Sheikh Dhahabu: Uislamu umekamilika, hakuna nafasi ya kuongeza wala kupunguza



### MASJID AN-NABAWI

Imam Masjid Nnabawi: Elimu ijenge maarifa, tabia na maadili



## Ruto awafukuza wageni kufanya biashara ndogo Kenya

المؤسسة الإسلامية

The Islamic Foundation

إنا لله وإنا إليه راجعون

Mwenyekiti wa Taasisi ya
The Islamic Foundation **Aref Nahdi**
kwa masikitiko na huzuni kubwa, anatoa
pole na rambirambi zake za dhati kwa
**Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan**
kufuatia msiba uliompata wa
kuondokewa na mwenza
wake mpendwa.

//////////////////////



tvImaan Tanzania
Radio Imaan FM
IMAAN NEWSPAPER

@islamicftz // @tvimaantz // @radioimaanfm
www.islamicftz.org






NA MWANDISHI WETU

# Mzee Ameir: Maisha ya utulivu, aondoka, akiacha alama zake

Viongozi mbalimbali wa Serikali, dini na vyama vya siasa wamehudhuria mazishi ya Hafidh Ameir Hassan, mume wa Rais Samia Suluhu Hassan, yaliyofanyika jana Kizimkazi, Mkoa wa Kusini Unguja, katika tukio lililokusanya viongozi wakuu wa Tanzania na wawakilishi wa mataifa jirani.



Marehemu Hafidh alifariki dunia jana saa mbili asubuhi katika Hospitali ya Kumbukumbu ya Emilio Mzena, Zanzibar, alipokuwa akitibiwa ugonjwa wa moyo.

Mazishi yake yalifanyika saa 10 jioni Kizimkazi, ambako alizikwa mbele ya ndugu, jamaa, viongozi na wananchi. Swala ya maiti iliongozwa na Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kaabi.

Hafidh ameacha wajane wawili, watoto wanne na wajukuu 15.

Miongoni mwa viongozi waliohudhuria mazishi hayo ni Makamu wa Rais, Deogratius Ndejembi; Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Mwinyi; na Waziri Mkuu, Mwigulu Nchemba.

Wengine ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah; Rais mstaafu wa Tanzania, Jakaya Kikwete; Rais mstaafu wa Zanzibar, Amani Abeid Karume; Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk Ali Mohamed Shein; na Makamu wa Kwanza wa Rais mstaafu wa Zanzibar, Othman Masoud Othman.

Mazishi hayo pia yalihudhuriwa na Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Stephen Wasira; Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Abdi Mahmoud Abdi, pamoja na mawaziri na manaibu waziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

## Mwinyi atoa pole

Katika salamu zake za pole kwa Rais Samia, Dk Mwinyi alisema amepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo hicho na kuungana na Rais, familia, ndugu na jamaa katika kipindi cha majonzi.

"Msiba huu ni mkubwa kwa familia na wote waliokuwa karibu na marehemu, hivyo namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie Rais Samia pamoja na familia yake subira, nguvu na faraja katika kipindi hiki kigumu," alisema.

Rais wa Kenya, William Ruto, alisema Rais Samia amempoteza mwenza wa maisha, watoto wake wamepoteza baba mpendwa na Tanzania imepoteza mwana wake mashuhuri.

Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema, alisema nchi yake iko pamoja na familia ya kwanza na Watanzania wote katika kipindi hicho kigumu.

Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye, naye alitoa pole kwa Rais Samia na familia yake, akiwaombea faraja na nguvu.

"Na Mungu aijalie roho ya Hafidh Ameir Hassan ipumzike kwa amani ya milele," alisema.

## Alama katika kilimo

Kwa waliowahi kufanya kazi naye, Hafidh anaondoka akiwa ameacha historia katika sekta ya kilimo, hasa uendelezaji wa zao la nazi, pamoja na mchango katika kuwajenga wataalamu waliokuja kulitumikia Taifa.

## Aref Nahdi (Mwenyekiti, The Islamic Foundation), Viongozi Afrika wamfariji Rais Samia

**Mwenyekiti wa The Islamic Foundation, Aref Nahdi, naye ametuma salamu za rambirambi kwa Rais Samia, familia yake na Watanzania kufuatia msiba huo.**

**Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Mahmoud Ali Youssouf, pia ametuma salamu za pole kwa Rais Samia, familia yake na Watanzania.**

**Salamu nyingine zimetolewa na viongozi mbalimbali wa ndani na nje ya nchi, wakiwemo Rais William Ruto wa Kenya na Rais Evariste Ndayishimiye wa Burundi, walioeleza mshikamano wao na Tanzania katika kipindi hiki cha majonzi.**

**Hafidh na Rais Samia walifunga ndoa mwaka 1978 na wamejaaliwa watoto wanne ambao ni Ameir, Abdul, Ahmed na Wanu Hafidh Ameir.**

**Wanu ni Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.**

**Kitaaluma, Hafidh alikuwa mtaalamu wa kilimo na aliwahi kuitumikia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika kipindi ambacho mkewe amekuwa katika uongozi wa juu wa nchi, aliendelea kuishi maisha ya faragha na kujiepusha kwa kiasi kikubwa na shughuli za kisiasa za hadharani.**

Hafidh aliyewahi kuwa mtumishi wa Serikali katika Wizara ya Kilimo na mwalimu katika Chuo cha Kilimo Kizimbani, alijenga jina katika ufundishaji na utaalamu wa kilimo.

Kassim Biwi, aliyewahi kufanya naye kazi, alisema marehemu anakumbukwa kama mtaalamu mstaafu wa zao la nazi na mkufunzi wa zamani wa Chuo cha Kilimo Kizimbani.

"Huyu ni mtaalamu mstaafu wa zao la nazi na mkufunzi wa zamani katika Chuo cha Kilimo cha Kizimbani," alisema.

إِنَّا لِلَّٰهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ




# MATUKIO KATIKA PICHA

**Na Ofisi Makamu wa Rais**

## Shughuli ya maziko ya aliyekuwa mume wa Rais Samia Suluhu Hassan iliyofanyika Kizimkazi mjini Unguja








UKHTI FATIMA SS

# Sheikh Bane ausia wanawake wa Kiislamu: Jitambueni, jithaminini

Sheikh Twaha Suleiman Bane amewataka wanawake Waislamu kutambua thamani na nafasi kubwa waliyopewa na Mwenyezi Mungu, wasijione wanyonge wala kuruhusu wengine kuwashusha hadhi tofauti na heshima waliyopewa na Uislamu.

Sheikh Bane alitoa wosia huo katika mhadhara uliofanyika katika Viwanja vya Judo, Pemba, ikiwa ni sehemu ya kampeni ya kuhamasisha Waislamu kuhusu ibada ya Hijja.

Sheikh Bane na viongozi wenzake wa taasisi ya iTravel Hajj and Umrah wapo Pemba katika ziara ya kuelimisha umma na kuhamasisha kuhusu ibada ya Hijja, nguzo ya tano ya Uislamu.

"Usia wangu kwa akinamama wajitambue, mjue thamani yenu, mjue nafasi yenu, msijione wanyonge," alisema Sheikh Bane.

Alisema Uislamu umempa mwanamke nafasi kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu, akirejea Surat Al-Ahzab aya ya 35 ambayo inawataja wanaume na wanawake kwa pamoja katika sifa mbalimbali za uchamungu na kuwaahidi msamaha na ujira mkubwa.

Aya hiyo inawataja Waislamu wanaume na wanawake, Waumini wanaume na wanawake, watiifu, wakweli, wenye subira, wanyenyekevu, watoao sadaka, wafungao, wanaojilinda na wanaomkumbuka Allah kwa wingi.


Sheikh Bane alisema umuhimu wa mwanamke unaonekana pia katika nafasi yake ya kuzaa na kulea jamii.

"Sisi sote tumepita katika miili yenu," alisema.

"Wanawake wakinyooka, jamii nzima itanyooka. Wao ni shule kamili. Wao ni waheshimiwa, ujanja wetu wote [wanaume] tumepita kwao... Ni wao pia [kama wake] ndio wanatupatia wanaume utulivu unaotuwezesha kufanya mambo makubwa."

Alisema ndio maana anapata matumaini anapofika katika mihadhara na kukuta wanawake wengi.

"Ndiyo maana sisi tunapokwenda kwenye vikao kama hivi tukikuta idadi kubwa ya wakinamama tunapata matumaini, kwa




sababu ujumbe tutakaokuwa tunautoa utakuwa umefika katika mikono salama ambao ni wakinamama," alisema.

Lakini mfano mkubwa alioutumia kuonesha nafasi ya mwanamke ulikuwa wa Hajar, mama wa Nabii Ismail, ambaye historia yake imefungamana moja kwa moja na Makka na ibada ya Hijja.

Sheikh Bane aliwakumbusha wanawake mazingira ambayo Hajar aliachwa akiwa na mwanawe mdogo katika bonde la Makka wakati huo likiwa eneo kavu lisilo na mimea wala mazingira ya kawaida ya maisha.

Qur'an inanukuu dua ya Nabii Ibrahim akisema: "Mola wetu! Hakika nimewaweka baadhi ya kizazi changu katika bonde lisilokuwa na mimea, karibu na Nyumba Yako Tukufu..." [Qur'an, 14:37].

"Kama Allah asingefaradhisha Hijja basi tungesema Hijja mwenyewe ni mwanamke. Makka lilikuwa jangwa lisilokuwa na chochote, eneo la bonde, jangwa halina mmea wowote, zile sababu za kuishi mtu haziko. Hakuna matunda, hakuna maua, hakuna miti. Nani wa kwanza kukaa pale? Alikuwa Hajar," alisema Sheikh Bane.

Alisema Hajar aliachwa pale pamoja na kichanga chake Ismail, katika mazingira ambayo kwa macho ya kawaida hayakuwa na matumaini ya maisha.

"Hatimaye ikawa wao ndio sababu ya kuwepo hiyo Makka na hatimaye kuwa jiji kubwa lenye heshima yake. Lakini Ibrahim alitokomea alikokujua, alimuacha huyu kichanga na mama yake pale akiomba kwa Allah alete msaada wake," alisema.

Katika kutafuta maji kwa ajili ya mwanawe, Hajar alihangaika kati ya vilima vya Swafa na Marwa, tukio ambalo limebaki kuwa sehemu ya ibada inayotekelezwa na mahujaji hadi leo.

Qur'an inasema: "Hakika Swafa na Marwa ni miongoni mwa alama za Allah. Basi anayehiji Nyumba hiyo au kufanya Umra, si kosa kwake kuvizunguka..." [Qur'an, 2:158].

Sheikh Bane alisema: "Swafa na Marwa Allah ameiweka kuwa nguzo ya Hijja ili iwe kumbukizi ya huyu mwanamke aliyekuwa akitangatanga. Allah amesema na nyinyi lazima mtembee kutoka Swafa kwenda Marwa mara 7 tena sio hiari, lazima."

Kwa mtazamo wake, historia hiyo pekee inatosha kumfanya mwanamke Muislamu asijione mdogo.

"Wito wangu kwa wanawake watambue nafasi yao, wajiheshimu na wasikubali kudhalilishwa," alisema Sheikh Bane.

Akaongeza kuwa Hijja ni ibada ya Waislamu wote, lakini kama kungekuwa na kundi ambalo lingeweza kujivunia nafasi ya kipekee katika historia yake, basi wanawake wangekuwa na hoja kubwa ya kufanya hivyo.

# Waislamu waaswa waache israfu, waipe Hijja kipaumbele



Sheikh Twaha Suleiman Bane amewataka Waislamu kupanga upya vipaumbele vya matumizi yao, akisema baadhi yao wana uwezo wa kutekeleza Hijja lakini fedha zao zinaishia katika matumizi yasiyo ya lazima.

Alisema changamoto kubwa si ukosefu wa uwezo wa kifedha pekee, bali pia uelewa mdogo kuhusu nafasi ya Hijja na namna Waislamu wanavyopanga matumizi yao.

Sheikh Bane alisema hayo katika mhadhara ulioandaliwa na iTravel Hajj and Umrah katika Viwanja vya Judo, Pemba, ikiwa ni mwendelezo wa kampeni ya taasisi hiyo ya kuhamasisha utekelezaji wa ibada ya Hijja.

Akizungumzia mafanikio ya kampeni hiyo tangu ilipoanza takribani miaka mitatu iliyopita, alisema: "Si makubwa sana lakini si ya kupuuzwa."

Kwa mujibu wake, Tanzania imepewa mgao mkubwa wa idadi ya mahujaji kuliko inayokwenda sasa. Alisema licha ya nchi kuwa na mgao wa mahujaji 25,000, huko nyuma idadi iliyokuwa ikisafiri ilikuwa takribani 3,000, wakati katika Hijja iliyopita ilifikia karibu 5,000 jambo linaloonesha mabadiliko chanya.

Hata hivyo, Sheikh Bane alisema hawezi kuthibitisha kwamba ongezeko hilo limesababishwa na kampeni zao pekee, ingawa anaamini juhudi za uhamasishaji zimechangia.

Alisema moja ya mambo waliyoyagundua katika kampeni hiyo ni kuwepo kwa Waislamu wenye uwezo wa kifedha ambao hawakuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu wajibu wa Hijja.

## Sheikh Bane: Wasioswali ni Waislamu 'toleo jipya', Mtume angewashangaa!

**Sheikh Twaha Suleiman Bane ameeleza kusikitishwa na kuwepo kwa watu wanaojitambulisha kuwa Waislamu lakini hawatekelezi Swala, akisema hali hiyo ni miongoni mwa changamoto zinazopaswa kuitafakarisha jamii ya Kiislamu.**

**Akizungumza katika mhadhara uliofanyika Viwanja vya Judo, Pemba, Sheikh Bane alihoji namna mtu anavyoweza kujinasibisha na Uislamu lakini akaacha Swala. "Hivi hakuna wenzetu tunaowatambua kama Waislamu lakini hawaswali? Wako tele," alisema.**

**Sheikh Bane aliendelea kukosoa hali hiyo kwa maneno makali, akisema: "Wako tele ambao wanajifanya Waislamu lakini hawaswali. Nimesema wanajifanya kwa sababu ukiisoma dini hao wanajifanya."**

**Alisema kuzoeleka kwa hali hiyo katika jamii hakupaswi kufanya ionekane kuwa jambo la kawaida, akisisitiza umuhimu wa Waislamu kurudi katika utekelezaji wa mafundisho ya dini yao.**

**"Hawa ni toleo jipya la Waislamu. Kuwa mtu ni Muislamu lakini haswali kwa kweli ni toleo jipya kwa sababu hata Mtume angefufuliwa leo angeshangaa hawa ni kina nani!" alisema Sheikh Bane.**

Kwa mujibu wake, baadhi ya watu baada ya kuhudhuria mihadhara hiyo wameeleza kuwa hawakuwa wamefahamu kwamba, kutokana na uwezo wao wa kifedha, Hijja tayari ilikuwa wajibu kwao.

"Tunaamini tupo miongoni mwetu wengi, na sio wachache tunaweza kuhifadhi mapato ya kutekeleza Hijja kama sio huu basi mwakani. La msingi mtu unaweza ukaacha israfu, ukaacha ubadhirifu mkubwa ukaweza kufanya mambo yako ya maana," alisema.


Sheikh Bane alitumia mfano wa fedha nyingi zinazotumika katika baadhi ya sherehe za harusi, huku majukumu muhimu ya dini yakisogezwa pembeni.

"Shughuli moja inaweza kufanywa mahali pamoja kwa masaa machache unaweza kutumia milioni tatu au nne kwenye ukumbi wa kifahari. Fanya, lakini je, huna mengine muhimu katika Uislamu wako?" alihoji.

Alisema tatizo si kufanya sherehe au kutumia fedha katika mambo halali, bali ni kukosa uwiano wa vipaumbele mpaka matumizi ya anasa yakapewa nafasi kuliko wajibu wa msingi wa dini.

Kwa mtazamo wake, Muislamu mwenye kipato kinachomwezesha anaweza kuanza kuweka akiba kwa utaratibu na, badala ya kusubiri kuwa na fedha nyingi kwa wakati mmoja, kujiwekea lengo la kutekeleza Hijja katika mwaka mmoja au miaka michache ijayo.

Ujumbe mkuu wa Sheikh Bane kwa waumini ulikuwa mmoja: punguza israfu, panga matumizi na usiache mambo yenye umuhimu katika dini kwa sababu ya matumizi yanayoweza kupunguzwa.





NA MWANDISHI WETU

# TPA, DP World zaweka rekodi mpya Bandari ya Dar

## Mizigo sasa yafikia tani milioni 33.7

Bandari ya Dar es Salaam imevunja rekodi ya kushughulikia mizigo baada ya kufikisha tani milioni 33.7 katika mwaka wa fedha 2025/2026, huku uwekezaji katika teknolojia na miundombinu ukitajwa kuwa kichocheo kikuu cha ongezeko hilo.

Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Abed Gallus, alisema maboresho ya miundombinu, mifumo ya uendeshaji na ushirikiano na wadau yameongeza ufanisi wa shughuli za bandarini, ikiwemo kupunguza muda wa meli kusubiri na kuharakisha upakuaji wa mizigo.

Gallus alisema hayo alipokutana na wajumbe wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) pamoja na waandishi wa habari waliotembelea bandari hiyo hivi karibuni.

Alisema makubaliano ya uendeshaji kati ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) na DP World ni miongoni mwa hatua zilizochangia kuongeza ufanisi wa shughuli za bandari.

Takwimu zinaonesha kuwa tani milioni 33.7 zilizoshughulikiwa katika mwaka wa fedha 2025/2026 ni ongezeko la tani milioni sita ikilinganishwa na tani milioni 27.7 zilizoshughulikiwa mwaka uliotangulia. Ongezeko hilo ni kubwa zaidi ya wastani wa kihistoria wa ukuaji wa mizigo bandarini, ambao umekuwa takribani tani milioni 1.5 kwa mwaka.

Chini ya Mpango Mkuu wa Bandari ulioboreshwa, TPA inalenga kuongeza uwezo wa kushughulikia mizigo hadi tani milioni 62 kwa mwaka ifikapo 2031.

### Reli kupunguza mizigo barabarani

Sambamba na ongezeko la mizigo, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) imeanzisha Kituo cha Mizigo cha Malindi kwa lengo la kurahisisha usafirishaji wa mizigo kutoka bandarini kwenda maeneo ya ndani ya nchi.

Kituo hicho kitapokea mizigo moja kwa moja kutoka bandarini na kuiunganisha na mtandao wa reli kwa ajili ya usafirishaji kwenda mikoa ya bara, ikiwemo Morogoro, Dodoma na Shinyanga.

Gallus alisema Bandari ya Dar es Salaam ni mhimili muhimu wa uchumi wa taifa kutokana na nafasi yake kama lango kuu la biashara ya kimataifa kupitia bahari.

Kwa mujibu wa Gallus, zaidi ya asilimia 90 ya mizigo ya Tanzania inayosafirishwa kwa njia ya bahari hupitia Dar es Salaam. Aidha, bandari hiyo inachangia zaidi ya asilimia 40 ya mapato ya nchi yatokanayo na forodha.

Maboresho ya Bandari ya Dar es Salaam yanaenda sambamba na uwekezaji mkubwa wa Serikali ya Awamu ya Sita katika miradi ya miundombinu chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Miongoni mwa miradi hiyo ni uchimbaji wa kina cha njia ya maji ya bandari pamoja na ujenzi wa kituo cha kuhifadhi mafuta chenye thamani ya Sh678 bilioni, ulioanza mwaka 2024.

### Kurasini kukabiliana na msongamano

Wakati huohuo, Serikali imechukua hatua za kukabiliana na msongamano wa mizigo ya makontena kwa kubadili eneo la hekta 25 huko Kurasini kuwa Kurasini Logistics Park.

Kituo hicho kinatarajiwa kuanza kufanya kazi mwezi Novemba na kitakuwa na uwezo wa kushughulikia tani 700,000 za mizigo kwa mwaka. Mamlaka zinasema kituo hicho kitasaidia kupunguza msongamano katika maeneo ya kuhifadhia mizigo bandarini, pamoja na ucheleweshaji unaotokana na mifumo ya teknolojia ya habari.

# MIMBARI ZETU

IMEANDALIWA
Na Barnabas Mkwayu



## MASJID AL-HARAM
Imam wa Makka ataja funguo za riziki yenye baraka

## MASJID HAQQ
Sheikh Dhahabu: Uislamu umekamilika, hakuna nafasi ya kuongeza wala kupunguza

## MASJID AN-NABAWI
Imam Masjid Nnabawi: Elimu ijenge maarifa, tabia na maadili

## MASJID AL-HARAM



# Imam wa Makka ataja funguo za riziki yenye baraka

**MAKKA.** Imam na Khatibu wa Masjid al-Haram, Sheikh Osama Khayyat, amewataka Waislamu wote duniani kutafuta riziki zao kwa njia zilizo halali huku wakimtanguliza na kumtegemea Mwenyezi Mungu katika kila hatua, pamoja na kuchukua sababu zote zinazofaa za kimaisha.

Katika khutba ya Ijumaa iliyotolewa mjini Makka Septemba 4, 2026, Sheikh Khayyat alisisitiza kwa kina kuwa riziki, afya njema, na mahitaji mengine muhimu ya maisha ya kila siku ni miongoni mwa neema kubwa za Allah. Aliongeza kuwa uchamungu wa kweli na imani thabiti ndio nguzo na sababu kuu za kupata baraka tele na kuondokewa na dhiki au shida mbalimbali za kimaisha.

Alifafanua zaidi kuwa kufanya tawakkul ya kweli haimaanishi kukaa chini na kuacha juhudi binafsi, bali ni kuunganisha utegemezi wa moyo kwa Allah pamoja na kufanya kazi kwa bidii na juhudi kubwa. Sheikh Khayyat alitaja mambo kadhaa yanayoleta riziki yenye baraka ikiwemo toba ya kweli, dua za mara kwa mara, kuunga undugu, kutoa sadaka kwa wahitaji, na kuanza mapema shughuli za kutafuta riziki.

Pia, aliwaonya vikali Waislamu dhidi ya papara na haraka isiyo na tija katika kutafuta mali, mapato ya haramu, na miamala mibaya isiyoendana na maadili ya Kiislamu. Alikumbusha kuwa kutoa mali katika njia njema hakupunguzi utajiri au mali ya mtu, bali kuna malipo makubwa yaliyoahidiwa na Mwenyezi Mungu, akiwataka waumini kushikamana na njia halali.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Saudi Press Agency (SPA), ujumbe huo ulihimiza waumini kutokata tamaa wanapocheleweshewa riziki zao, bali waendelee kujitahidi, kuomba, na kushikamana na misingi ya uhalali.

## MASJID HAQQ




# Sheikh Dhahabu: Uislamu umekamilika, hakuna nafasi ya kuongeza wala kupunguza

**MOROGORO.** Mhadhiri wa Kiislamu, Sheikh Shaban Dhahabu, amewataka Waislamu kushikamana na Qur'an na Sunna, akisisitiza kuwa dini ya Uislamu ilishakamilishwa na Mwenyezi Mungu na hivyo haihitaji kuongezewa wala kupunguzwa.

Sheikh Dhahabu alitoa kauli hiyo wakati akizungumza katika khutba iliyofanyika Masjid Haqq, eneo la Karume mkoani Morogoro, ambapo alizungumzia madhara ya bidaa (uzushi katika mambo ya dini) na umuhimu wa kurejea katika mafundisho sahihi ya Uislamu.

Akirejea Qur'an, Sheikh Dhahabu alisema Mwenyezi Mungu anasema: "Leo nimekukamilishieni dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimekuridhieni Uislamu uwe dini yenu." [Qur'an, 5:3].

Kwa mujibu wa Sheikh Dhahabu, aya hiyo inaweka wazi kuwa Uislamu ni dini iliyokamilika, hivyo si sahihi kwa mwanadamu kujaribu kuongeza ibada au mafundisho ambayo hayakuwekwa katika dini hiyo.

Alisema Uislamu unapaswa kueleweka na kutekelezwa kwa kurejea Qur'an na Sunna, kwa ufahamu wa wema waliotangulia, akisisitiza kuwa kushikamana na misingi hiyo ndiyo njia ya kulinda usahihi wa dini.

"Uislamu ni dini ambayo ilishakamilika, haihitaji nyongeza, wala haihitaji kupunguzwa," alisema. Sheikh Dhahabu alisema suala la kuwakumbusha Waislamu madhara ya bidaa hakutokani na chuki, uadui au kutaka kuwagawa waumini, bali ni sehemu ya kutoa nasaha na kuwatakia kheri.

Alisema baadhi ya maonyo kuhusu uzushi katika dini yanaweza kuonekana kuwa makali, lakini lengo lake ni kuwaeleza Waislamu hatari inayoweza kutokana na kuingiza mambo mapya katika dini ya Mwenyezi Mungu.

## MASJID AN-NABAWI



# Imam Masjid Nnabawi: Elimu ijenge maarifa, tabia na maadili

**MADINA.** Imam na Khatibu wa Masjid an-Nabawi, Sheikh Dkt. Abdulbari bin Awadh Al-Thubaiti, amesema kwa msisitizo mkubwa kuwa elimu yenye manufaa ya kweli ndiyo msingi thabiti wa kujenga mtu mwema na kuandaa mustakabali mzuri wa jamii na taifa.

Katika khutba ya Ijumaa, Sheikh Al-Thubaiti alifafanua kuwa elimu haipaswi kuishia tu katika kazi ya kuhamisha maarifa ya vitabuni, bali lazima ijenge utu wa mwanadamu, ipandikize maadili mema, na iandae kizazi chenye uwezo wa dhati wa kuhudumia jamii. Alikumbusha kuwa neno la kwanza kushuka kupitia Wahyi mtukufu lilikuwa "Iqra" — Soma — akisema hilo linaonesha wazi nafasi kubwa sana ya elimu katika kujenga imani na kuongoza maisha ya mwanadamu.

Sheikh Al-Thubaiti alieleza wazi kuwa mwalimu ana jukumu kubwa zaidi ya kufundisha mtaala wa kawaida; anapaswa kuwa mlezi makini, mfano bora wa maadili, na chanzo cha hamasa kwa wanafunzi wake. Aliwataka walimu kuwa waadilifu, wenye subira, huruma, na upole katika utendaji wao, huku wanafunzi wakihimizwa kuheshimu walimu, kutumia vizuri muda wao wa masomo, na kuchagua marafiki wema wa kuandamana nao.

Alisema jamii nzima na vyombo vya habari vinapaswa kuinua hadhi ya elimu na kuwaheshimu walimu, kwa kuwa ni washirika muhimu sana katika kujenga vizazi vijavyo na mustakabali mwema. Pia alisisitiza kuwa teknolojia ya kisasa itumike kwa uangalifu mkubwa, kwa kuhakiki taarifa na vyanzo vyake, kutofautisha maarifa yenye manufaa na taarifa potofu, na kulinda daima dini, maadili, pamoja na utambulisho wa jamii nzima.

NA MWANDISHI WETU

# PM akataa misururu mirefu kusindikiza viongozi”



> “Kukagua darasa lililojengwa kwa Sh24 milioni mnaenda na magari 150 na gari la mbunge linakuwa la 151.”
>
> **Waziri Mkuu Mwigulu Nchemba**

Waziri Mkuu, Dk Mwigulu Nchemba, ameiagiza Serikali kupunguza misururu ya magari na watendaji wanaoambatana na viongozi katika ziara za kikazi, akisema utaratibu huo unaongeza matumizi yasiyo ya lazima ya fedha za umma.

Amesema endapo kiongozi anatembelea wilaya zote ndani ya mkoa mmoja, Mkuu wa Mkoa pamoja na Mkuu wa Wilaya inayotembelewa wanatosha kuambatana naye, badala ya watendaji wa mkoa mzima kusafiri katika kila wilaya.

Dk Mwigulu alitoa agizo hilo hivi karibuni jijini Dodoma katika hotuba yake ya kuhitimisha mkutano wa nne wa Bunge la 13, akitaja matumizi ya magari, mafuta, safari za ndani na nje, mikutano, warsha, makongamano na michakato ya bajeti kuwa miongoni mwa maeneo yanayopaswa kubanwa.

Alimtaka Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Profesa Rizik Shemdoe, kuwaelekeza wakuu wa mikoa na wilaya kupunguza idadi ya watendaji katika misafara ya viongozi.

“Unaenda kwenye mkoa A ambapo utaenda wilaya zote. Lakini kwenye wilaya zote watendaji wa mkoa mzima... wapo kwenye kila wilaya. Matokeo yake mnaenda kukagua darasa lililojengwa kwa Sh24 milioni mnaenda na magari 150,” alisema.

Dk Mwigulu alikosoa pia tabia ya ofisi kufungwa na watendaji kuacha majukumu yao ili kwenda kumpokea kiongozi, akisema Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya husika wanatosha katika ziara hizo.

Hatua hiyo inaendana na msimamo uliowahi kutolewa na Rais Samia Suluhu Hassan Aprili 8, 2026, wa kupunguza msafara wake kwa kutumia mabasi kusafirisha baadhi ya watendaji, hasa kwa lengo la kupunguza matumizi ya mafuta.

Hata hivyo, suala hilo si geni kwa Dk Mwigulu. Mwaka 2022, akiwa Waziri wa Fedha na Mipango, alitangaza mpango wa kupunguza matumizi ya Serikali katika magari, mafuta, vipuri na matengenezo, yaliyokuwa yakifikia Sh558.45 bilioni.

Akizungumza kuhusu utekelezaji, mchambuzi wa siasa, Dk Baraka Mfinanga, alisema Serikali inahitaji mfumo madhubuti wa kufuatilia maagizo hayo, kwa kuwa baadhi ya watendaji wamejengeka katika utamaduni wa kutumia misafara mikubwa kama ishara ya heshima kwa viongozi.

Said Majjid, mchambuzi mwingine wa siasa, alisema Serikali haiwezi kuhimiza wananchi kuwa na nidhamu ya matumizi huku yenyewe ikigharamia shughuli zisizo na tija.

Dk Mwigulu pia alitaka kupunguzwa kwa idadi ya watendaji wanaoshiriki michakato ya bajeti, akisema fedha zinazotumika zinaweza kuelekezwa katika elimu, afya na miundombinu.




## Rais Samia apunguza msafara, abane mafuta

**Rais Samia Suluhu Hassan Aprili 8, 2026 alitangaza kupunguza msafara wake kwa kutumia mabasi kusafirisha baadhi ya watendaji wanaoambatana naye, akilenga kupunguza matumizi ya mafuta na gharama za uendeshaji wa Serikali.**

# Ruto awafukuza wageni kufanya biashara ndogo

## MAAGIZO YA RUTO

**"Raia wa kigeni hawapaswi kushindana na Wakenya katika biashara ndogo ndogo. Biashara ndogo zinapaswa kuleta fursa kwa raia wa Kenya."**




## Sept 7

**Muda wa mwisho uliowekwa na Kenya kwa raia wa kigeni wanaojihusisha na uchuuzi na biashara ndogo ndogo kufunga biashara zao.**

KAULI ya Rais wa Kenya, William Ruto, ya kuwataka raia wa kigeni kuacha kufanya biashara ndogo ndogo nchini humo imezua mjadala kuhusu ushindani wa wafanyabiashara, ulinzi wa fursa kwa raia na nafasi ya wawekezaji wa kigeni katika uchumi wa Kenya.

Ruto alitoa msimamo huo Septemba 2, 2026, alipokutana na wafanyabiashara wa biashara ndogo, za kati na ndogo zaidi (MSMEs) katika Ikulu ya Nairobi, akisema biashara ndogo zinapaswa kutoa fursa kwa Wakenya badala ya wageni kushindana nao.

Rais huyo alisema Serikali yake haiwezi kuvutia wawekezaji wa kigeni kwa lengo la kuja kufanya biashara zinazoweza kufanywa na wafanyabiashara wa ndani, akisisitiza kuwa wageni wanapaswa kuelekeza mitaji yao katika uwekezaji unaozalisha ajira na kuongeza shughuli za kiuchumi.

"Raia wa kigeni hawapaswi kushindana na Wakenya katika biashara ndogo ndogo. Biashara ndogo zinapaswa kuleta fursa kwa raia wa Kenya," alisema Ruto.

Alisema kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara wa ndani kuhusu wageni wanaoingia katika biashara ndogo, zikiwamo shughuli za uchuuzi na uendeshaji wa maduka madogo, na hivyo kushindana moja kwa moja na Wakenya. Ruto alitoa mfano wa baadhi ya wageni wanaouza bidhaa kama mashuka na bidhaa nyingine kwa rejareja, akisema shughuli kama hizo zinapaswa kuwa fursa kwa wafanyabiashara wa Kenya.

Kutokana na msimamo huo, aliagiza hatua za kuanza kuwaondoa wageni wanaojihusisha na biashara hizo, huku utekelezaji ukitarajiwa kuanza Septemba 7.

Aidha, Ruto alisema tayari kuna muswada unaojadiliwa na Bunge unaolenga kuweka kisheria maeneo ya biashara ambayo yanapaswa kutengewa raia wa Kenya. Aliwataka viongozi na wadau kuhakikisha sheria hiyo inafunga mianya inayoweza kutumiwa na wageni kuendelea kufanya biashara zinazolengwa na zuio hilo.

Hatua hiyo imeibua mjadala mpana kuhusu namna Kenya inavyoweza kulinda wafanyabiashara wake wadogo bila kuathiri uwekezaji wa kigeni, ambao Serikali imeendelea kuutangaza kuwa muhimu katika kukuza uchumi na ajira.

Wanaounga mkono msimamo wa Ruto wanaona hatua hiyo inaweza kuwapa wafanyabiashara wa ndani nafasi kubwa zaidi katika sekta ya biashara ndogo, hususan vijana na wajasiriamali wanaotegemea biashara hizo kwa kipato.

Hata hivyo, wakosoaji wameibua hofu kuhusu namna utekelezaji utakavyofanyika, hasa kwa wageni ambao wana vibali na leseni halali za kufanya biashara nchini Kenya. Mashirika ya kiraia pia yameonya kuwa utekelezaji usio na uwiano unaweza kusababisha ubaguzi, unyanyasaji au kuongezeka kwa hisia za chuki dhidi ya wageni.

Mjadala huo umeongezeka zaidi baada ya Katibu Mkuu katika Wizara ya Mambo ya Nje ya Kenya, Korir Sing'Oei, kueleza Septemba 6 kuwa kauli ya Ruto haikupaswa kutafsiriwa kama marufuku ya jumla kwa wafanyabiashara wote wa kigeni nchini humo. Kwa sasa, mjadala unaendelea kuhusu mipaka kati ya kulinda fursa za wafanyabiashara wa ndani na kudumisha mazingira rafiki kwa uwekezaji wa kigeni, huku hatua za Serikali zikitarajiwa kufafanua zaidi aina ya biashara zitakazolengwa.

HABARI
DODOMA

NA MWANDISHI WETU

# Dkt. Mwigulu: Viongozi wekeni utaratibu kusikiliza kero za wananchi

Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Nchemba amewaagiza viongozi na watendaji wa Serikali kuweka utaratibu maalum wa kuwasikiliza wananchi, kutatua kero zao kwa wakati na kutoa mrejesho, akisisitiza kuwa hatua hiyo ni muhimu katika kuimarisha uwajibikaji na ufanisi wa utumishi wa umma.

Dkt. Mwigulu alitoa maagizo hayo Septemba 4, 2026 bungeni jijini Dodoma wakati akitoa hoja ya kuahirisha Mkutano wa Nne wa Bunge la 13.

Alisema viongozi na watendaji wanapaswa kutoka ofisini na kuwafuata wananchi katika maeneo yao, kusikiliza kero zao na kuzitafutia ufumbuzi, akisisitiza kuwa hatua hiyo ni sehemu ya msingi ya msimamo wa Serikali ya Awamu ya Sita wa kupeleka maendeleo yanayogusa maisha ya wananchi moja kwa moja.

"Watendaji wote wa Serikali lazima tuwe na utaratibu maalum wa kuwasikiliza wananchi, kutatua kero zao kwa wakati na kutoa mrejesho. Hii ni sehemu ya uwajibikaji wetu," alisema.

Dkt. Mwigulu pia alionya kuhusu matumizi yasiyo ya lazima katika shughuli za Serikali, akisema baadhi ya fedha zinazotumika katika mikutano na shughuli nyingine zinaweza kuelekezwa kwenye miradi ya maendeleo yenye manufaa ya moja kwa moja kwa wananchi.

Alitoa mfano wa shilingi bilioni 20 zinazohitajika kwa ujenzi wa madarasa, akisisitiza umuhimu wa kuchunguza kwa umakini matumizi ya fedha za Serikali ili kuhakikisha rasilimali zinaelekezwa kwenye maeneo yenye tija na yanayogusa moja kwa moja maisha ya wananchi.

Akizungumzia gharama zinazotokana na ziara za viongozi, Waziri Mkuu alisisitiza umuhimu wa kupunguza misafara mikubwa isiyo na tija, akieleza kuwa ziara hizo hazipaswi kuathiri shughuli za Serikali katika maeneo wanayopita.

Aidha, aliwataka watendaji wa Serikali kubaini maeneo mengine yanayoweza kupunguza matumizi bila kuathiri ufanisi wa utoaji wa huduma kwa wananchi. Alitaja maeneo hayo kuwa ni pamoja na matumizi ya shajara, gharama za safari za nje, michakato ya bajeti kwa kupunguza idadi ya watumishi wanaoshiriki, pamoja na gharama za mikutano, warsha, makongamano na safari nyingine za kikazi.

# Watafiti watwikwa mzigo wa malezi ya Gen Z



Watafiti kutoka taasisi mbalimbali, wakiwamo wanaojihusisha na utetezi wa haki za watoto, wametakiwa kufanya tafiti zitakazobaini mbinu bora za malezi zinazokidhi mahitaji ya watoto katika mazingira ya sasa yanayobadilika kwa kasi.

Wito huo umetolewa Septemba 4, 2026 jijini Mwanza na Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Dkt. Silas Wambura, aliyemwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Eliakim Maswi katika ufunguzi wa mdahalo wa wadau kuhusu kuimarisha afua za malezi nchini.

Dkt. Wambura alisema tafiti hizo ni muhimu katika kuhakikisha kuwa maamuzi, sera na mikakati ya malezi inazingatia mazingira halisi wanayokulia watoto wa kizazi cha sasa, badala ya kutegemea mifumo ambayo huenda isiendane na mabadiliko yanayoendelea katika jamii.

Alisema watoto wa sasa wanakua katika mazingira tofauti na zamani, huku mitandao ya kijamii na matumizi ya vifaa vya kidijitali yakiwa sehemu ya maisha yao ya kila siku. Alitaja suala la umri sahihi wa kuwapa watoto simu za mkononi kuwa miongoni mwa maeneo yanayohitaji utafiti zaidi.

"Tumekuwa tukitofautiana kuhusu kama ni muhimu kumpa mtoto ambaye bado yuko sekondari simu au asubiri. Kila mtu ana mtazamo wake. Mwenzangu alijenga hoja kwamba ni vizuri watoto wapate exposure, lakini waongozwe namna ya kutumia simu," alisema.

Dkt. Wambura alisema mabadiliko ya kiuchumi nayo yanaendelea kuathiri maisha ya watoto, akibainisha kuwa baadhi yao wanaanza shule wakiwa na umri mdogo, wanamaliza masomo mapema na baadaye kuingia katika maeneo ya kazi wakiwa bado vijana.

UKHTI FATIMA SS




# Soko la halal linavyovuka mipaka ya chakula na nyama

Biashara ya halal duniani inaingia katika hatua mpya, ikipanuka kutoka mtazamo wa kawaida wa vyakula na nyama kwenda katika mfumo mpana wa uchumi unaohusisha bidhaa, huduma, teknolojia, viwanda na biashara ya kimataifa.

Kwa muda mrefu, neno halal lilihusishwa zaidi na nyama iliyochinjwa kwa mujibu wa mafundisho ya Kiislamu.

Lakini hali hiyo inabadilika kwa kasi. Leo, bidhaa za vyakula vilivyosindikwa, viambato vya chakula, sukari, nafaka, vipodozi, dawa, kemikali na bidhaa nyingine nyingi zinaingia katika mnyororo wa biashara ya halal.

Mabadiliko hayo yanaifanya halal isiwe tu suala la kidini, bali pia sehemu muhimu ya ushindani wa biashara katika masoko ya kimataifa.

Kwa kampuni zinazotafuta masoko mapya, uthibitisho wa halal (halal certification) unazidi kuwa nyenzo ya kimkakati. Kampuni haitakiwi tena kusubiri mnunuzi aombe cheti cha halal. Badala yake, suala hilo linaweza kuingizwa mapema katika mipango ya uzalishaji, uteuzi wa malighafi, wasambazaji, uhifadhi, usafirishaji na udhibiti wa ubora.

Kwa maana hiyo, halal inakuwa sehemu ya mkakati wa kuingia katika masoko mapya. Kinachoifanya biashara hii kuwa muhimu zaidi ni suala la uaminifu.

Mlaji Muislamu anahitaji kuwa na uhakika kwamba bidhaa si halal kwa jina pekee, bali mchakato mzima wa uzalishaji, uhifadhi na usambazaji umefuata masharti yanayotakiwa. Hivyo, uwezo wa kufuatilia bidhaa ilikotoka (traceability), uwazi na udhibiti wa mnyororo wa uzalishaji vinazidi kuwa muhimu.

Sifa hizi pia zinavutia walaji wengine wasiokuwa Waislamu ambao wanazidi kuzingatia usalama, uwazi na uadilifu katika uzalishaji wa bidhaa wanazonunua.

Sekta ya halal yenyewe nayo inabadilika. Nchi zinazoagiza bidhaa zinaimarisha viwango, mifumo ya utambuzi wa vyeti na usimamizi wa taasisi zinazotoa uthibitisho. Wakati huo huo, sekta mpya za biashara zinaanza kutambua ukubwa wa soko hili.

Hali hiyo inalazimisha taasisi zinazotoa vyeti vya halal kujiendesha kitaalamu zaidi, kutumia teknolojia, kuimarisha utawala bora na kufuata viwango vinavyotambuliwa kimataifa.

Kwa hiyo, uthibitishaji wa halal haupaswi kutazamwa kama hatua ya mwisho ya kuweka muhuri kwenye bidhaa. Unapaswa kuwa sehemu ya mfumo mzima unaoiandaa biashara kuelewa soko, kufuata masharti na kujenga uaminifu kwa walaji.

Kadiri biashara ya kimataifa inavyozidi kuunganishwa, halal inaweza kuwa daraja kati ya wazalishaji na mamilioni ya walaji wanaotafuta bidhaa zinazoendana na imani, maadili na matarajio yao.

Fursa kubwa inayokuja, hivyo, si kuuza bidhaa nyingi zaidi pekee. Ni kujenga mfumo wa biashara unaounganisha ubora, uwazi, uaminifu na uwezo wa kufikia masoko mapya.

## Uingereza yaongoza fedha za Kiislamu nchi za Magharibi

**UINGEREZA imeendelea kuwa kitovu kikuu cha fedha za Kiislamu miongoni mwa nchi za Magharibi na zisizo wanachama wa Jumuiya ya Ushirikiano wa Kiislamu (OIC), licha ya soko lake la ndani kubaki dogo.**

**Kwa mujibu wa Fitch Ratings, nafasi hiyo inachangiwa na nguvu ya London katika masoko ya sukuk, uwepo wa benki za Kiislamu, mifuko ya uwekezaji, taasisi zisizo za kibenki na kampuni za teknolojia ya fedha.**

**Hadi nusu ya kwanza ya mwaka 2026, Soko la Hisa la London lilihifadhi zaidi ya nusu ya sukuk zote za kimataifa zinazotolewa kwa dola za Marekani, kutoka takribani asilimia 42 mwaka uliotangulia. Uingereza pia ina benki tano kamili za Kiislamu, ambazo kwa pamoja zilikuwa na mali zenye thamani ya dola bilioni 12.5 mwishoni mwa 2025, ongezeko la asilimia 7 kwa mwaka. Hata hivyo, sekta hiyo bado inawakilisha chini ya asilimia moja ya mali zote za mfumo wa benki nchini humo.**

## Benki za Kiislamu zazidi kuwavutia wasiokuwa Waislamu

**BENKI za Kiislamu zinaendelea kuvutia wateja wasiokuwa Waislamu kutokana na msisitizo wake katika maadili, uwazi, uwajibikaji na matumizi ya fedha yenye kuzingatia manufaa ya jamii.**

**Katika makala ya Ameen Hassen, Mkuu wa Huduma za Benki kwa Mujibu wa Shariah katika Standard Bank iliyochapishwa wiki hii, amesema ongezeko hilo linaonyesha mabadiliko ya namna watu, wafanyabiashara na wawekezaji wanavyofanya maamuzi ya kifedha. Amesema ingawa benki za Kiislamu zinabaki kujengwa juu ya misingi ya Shariah, baadhi ya kanuni zake zinafanana na malengo ya uwekezaji unaozingatia mazingira, jamii na utawala bora, maarufu kama ESG.**

**Miongoni mwa misingi hiyo ni uwazi, uwajibikaji, haki, utawala bora na uwekezaji unaolenga shughuli halisi za kiuchumi.**

**Kwa wateja Waislamu, kufuata masharti ya Shariah bado ndiyo sababu kuu ya kuchagua huduma hizo, lakini Hassen anasema kuvutiwa kwa wateja wengine kunafungua nafasi mpya ya ukuaji. Alieleza kuwa fursa hiyo ni muhimu zaidi Afrika, ambako kuna mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya miundombinu, biashara ndogo na za kati pamoja na ujasiriamali.**

NA UKHTI FATIMA



# Kwa nini mjasiriamali anapaswa kusafiri

**WAJASIRIAMALI wengi huona kusafiri kama kitu cha kufanya baada ya biashara kusimama vizuri. Kwanza kazi, baadaye safari.**

**Lakini mtazamo huo unaweza kukunyima moja ya shule muhimu za biashara. Safari, hasa inayokupeleka katika mazingira mapya, si mapumziko pekee. Inaweza kukupa mawazo mapya, kukuonyesha masoko usiyoyajua, kukutanisha na watu wapya na kukusaidia kuitazama biashara yako kwa macho tofauti.**

**Kwa Muislamu, safari pia inaweza kuwa nafasi ya kutafakari dunia na kujifunza. Qur'an inatuhimiza kutembea katika ardhi na kutazama namna uumbaji ulivyoanza: "Tembeeni katika ardhi, kisha tazameni jinsi alivyoanzisha uumbaji..." [Qur'an, 29:20].**

**Hivyo, unaweza kusafiri kwa mapumziko, lakini pia ukarudi na maarifa.**

**Na si lazima uende Ulaya, Marekani au Asia. Hata kwenda mkoa mwingine, mji mwingine, maonesho ya biashara au mkutano katika mazingira usiyozoea kunaweza kukufundisha mengi.**

## Safari hupanua namna unavyofikiri

Ukikaa sehemu moja muda mrefu, ni rahisi kuamini kuwa namna unavyofanya mambo ndiyo ya kawaida au bora zaidi.

Lakini ukisafiri unaona watu wakitatua matatizo yale yale kwa njia tofauti. Unaona namna biashara zinavyopanga maduka, kuhudumia wateja, kutangaza bidhaa, kutumia teknolojia au kuweka bei.

Mjasiriamali makini haendi tu kupiga picha. Anaangalia. Anauliza: "Kwa nini hapa wanafanya hivi? Kuna kitu naweza kujifunza?"

Katika Uislamu, kutafuta maarifa ni jambo lenye thamani. Qur'an inatufundisha kuomba: "Mola wangu, niongezee elimu." [Qur'an, 20:114].

Safari inaweza kuwa sehemu ya elimu hiyo.

## Unaanza kuwaelewa wateja kwa upana

Biashara ni watu. Tatizo ni kwamba wakati mwingine tunawafahamu vizuri watu wanaofanana nasi pekee.

Safari inakuweka karibu na watu wenye tamaduni, kipato, lugha, vyakula na mitindo tofauti ya maisha. Hapo unaweza kugundua kwamba kile unachodhani "kila mtu anataka" si kweli.

Hata ndani ya Umma wa Kiislamu, safari inaweza kukuonyesha tofauti kubwa za mila, vyakula, mavazi na namna za kufanya biashara huku watu wakikusanywa na imani moja.

Mjasiriamali anayejifunza kuelewa tofauti hizo anakuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kuwafahamu wateja wake.

## Unakutana na watu ambao usingekutana nao

Mteja wa kesho, mshirika wa biashara, mshauri au mtu atakayekupa wazo muhimu anaweza kuwa nje ya mzunguko wako wa kawaida.

Maonesho, mikutano, semina na hata mazungumzo ya kawaida njiani yanaweza kuzaa mahusiano yenye thamani. Lakini hilo linahitaji uwe tayari kuzungumza na watu.

Usafiri ukiishia hotelini na kwenye simu, unaweza kurudi na picha nyingi lakini maarifa machache. Jifunze kusalimia, kusikiliza na kuuliza.

Kwa Muislamu, hili linaweza kwenda sambamba na adabu nzuri, uaminifu na kuwakilisha vizuri maadili ya dini yake popote anapokwenda.

## Safari inakufundisha kubadilika

Safari haiendi kila wakati kama ulivyopanga. Usafiri unaweza kuchelewa. Njia ikabadilika. Lugha ikawa kikwazo. Kitu ulichotegemea kisipatikane.

Unalazimika kutafuta suluhisho. Huo ndio uwezo anaouhitaji mjasiriamali.

Wateja hubadilika. Bei hupanda. Teknolojia mpya inaingia. Washindani wanakuja. Mjasiriamali anayejifunza kuzoea mazingira mapya anakuwa tayari zaidi kubadilisha njia bila kuacha lengo.

## Unaweza kuona fursa mpya

Safari hukuweka mbele ya bidhaa, huduma na mifumo ya biashara ambayo hujawahi kuiona.

Unaweza kuona huduma inayofanya vizuri mahali fulani na kujiuliza kama inaweza kurekebishwa ili itatue tatizo katika soko lako. Au unaweza kuona tatizo ambalo hakuna aliyelitatua vizuri.

Mjasiriamali huona zaidi ya kile kilicho mbele ya macho yake. Anauliza: "Kuna hitaji gani hapa? Watu hawa wanapata shida gani? Naweza kuongeza thamani gani?"

Hapo safari inageuka kuwa utafiti wa soko.

## Kubadilisha mazingira kunaweza kufungua akili

Ujasiriamali unaweza kuwa kazi ya saa zote. Kuna wateja, fedha, wafanyakazi, simu na matatizo ya kila siku. Unaweza kuwa bize sana katika kuendesha biashara kiasi cha kukosa muda wa kufikiri kuhusu biashara yenyewe.

Safari inaweza kukutoa kwa muda katika mzunguko huo.

Unaanza kujiuliza: Tunafanya nini kwa mazoea? Tunahitaji kubadilisha nini? Biashara hii inaelekea wapi?

Wakati mwingine akili inahitaji umbali kidogo ili kuona picha kubwa.

## Safari inaweza kukufundisha maana ya mafanikio

Unaposafiri na kuona namna watu tofauti wanavyoishi, unaweza kugundua kwamba mafanikio hayana maana moja. Kwa mmoja ni fedha nyingi. Kwa mwingine ni biashara inayompa muda wa familia. Kwa mwingine ni kuajiri watu. Kwa mwingine ni kutatua tatizo la jamii.

ربيع أول

HABARI MASHARIKI YA KATI

NA Mahmoud Nyamguma




# Hamas yalaani mkakati wa Israel kuhamisha Wapalestina Gaza

Hamas imezitaka nchi za Kiislamu kuchukua hatua za haraka na za pamoja kuzuia mpango wa Israel wa kuwahamisha kwa nguvu zaidi ya Wapalestina milioni 2 kutoka Ukanda wa Gaza.

Muslim Network TV imemnukuu Msemaji wa Hamas, Hazem Qassem, akisema mpango huo hayo unadhihirisha uovu wa utawala wa Kizayuni unaolenga kuwafuta Wapalestina katika ardhi yao ya kihistoria.

Alitaka nchi za Kiislamu kutumia ushawishi wao wa kidiplomasia na kiuchumi ili kusimamisha jinai hiyo inayokiuka kikamilifu Mkataba wa Geneva unaopiga marufuku uhamishaji wa raia katika maeneo yanayokaliwa kwa mabavu.

Mpango huo hatari uliowasilishwa na waziri mwenye msimamo mkali wa Usalama wa Ndani wa Israel, Itamar Ben-Gvir, unalenga kuwahamisha Wapalestina 250,000 katika mwaka wa kwanza na kumaliza idadi iliyobaki ya wakazi milioni 2 ndani ya miaka sita ijayo kupitia kile anachokiita "uhamiaji wa hiari".

Huu si mpango wa hiari bali ni muendelezo wa mkakati wa utawala huo wa kutumia sera za kimabavu, kubomoa miundombinu ya afya na maji, na kuweka vizuizi ili kuifanya Gaza isiweze kukaliwa na watu.

Hali hii inashabihiana kikamilifu na maafa ya Nakba ya mwaka 1948, ambapo mamia kwa maelfu ya Wapalestina walifukuzwa kwa mabavu katika ardhi zao.

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
0789 201383

# Tusiache kuwaombea nusra ndugu zetu wa Gaza

Katika kile ambacho Israel ilikiita operesheni ya kijeshi ya ardhini ya kumkamata afisa wa ngazi ya juu wa Hamas, wiki iliyopita ndege zake za kivita zilifyatua takribani makombora 12 karibu na eneo la Katiba, lililopo magharibi mwa Jiji la Gaza na kusababisha vifo vya watu wanne, wakiwamo watoto wawili.

Maofisa wa afya wa Palestina pamoja na kikosi cha ulinzi wa kiraia walisema watu wengine wanane walijeruhiwa katika mashambulizi hayo.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya ya Gaza inayoongozwa na Hamas, hadi sasa zaidi ya Wapalestina 73,470 wameuawa katika Ukanda wa Gaza tangu kuanza kwa vita mnamo Oktoba 7, 2023, huku zaidi ya 174,540 wakijeruhiwa.

Takwimu hizi zinaonesha ni kwa kiasi gani Israel imedhamiria kuitwaa ardhi yote ya Palestina na kuifuta kabisa jamii ya Waarabu ambao ndio wenye ardhi hiyo. Israel inafanya unyama wote huo kwa madai ya kujibu mashambulizi ya kundi la Hamas, madai ambayo hayana mashiko asilani.

Ukweli utabaki pale pale kwamba Hamas inapigana kuwaondoa wavamizi katika ardhi yao baada ya juhudi za kidiplomasia kushindwa kwa miaka mingi kuleta suluhu ya kudumu.

Kinachotia uchungu zaidi ni kwamba mataifa makubwa duniani, yakiongozwa na Marekani, hayajaishia tu kufumbia macho dhuluma hiyo, bali yamechagua kuisitiri na kuipa Israel msaada unaoiwezesha kuendelea na hujuma hizo.

Waislamu wa Gaza wanastahili amani, utulivu na fursa ya kujenga upya maisha na makazi yao. Hata hivyo, malengo hayo hayawezi kufikiwa ikiwa Jumuiya ya Kimataifa itaendelea kufumbia macho uporaji wa ardhi yao na kulazimishwa kuondoka katika makazi yao.

Kadhalika, suluhisho la kudumu haliwezi kupatikana bila kushughulikia masuala ya msingi yanayochochea mzozo huo, yakiwamo haki za Wapalestina, hadhi ya ardhi wanayoishi pamoja na usalama na ustawi wao.

Dunia haipaswi kuendelea kufumbia macho mateso ya watu wa Gaza. Kila kifo cha raia, kila mtoto anayempoteza mzazi, kila familia inayolazimika kuacha makazi yake na kila hospitali inayokabiliwa na changamoto katika kuwahudumia majeruhi, vinapaswa kuwa ukumbusho wa gharama kubwa inayotokana na mzozo huu usiomithilika.

Tuguswe na mateso yanayowakabili ndugu zetu hawa na tutafakari namna ya kuwasaidia kwa hali na mali. Wenye uwezo wa kifedha wawachangie, na wanaopata fursa katika majukwaa makubwa wawasimamie kwa kuwasemea na kupaza sauti kuhusu madhila wanayopitia. Lakini kuna jambo moja ambalo kila mmoja wetu anaweza kulifanya bila kujali uwezo wake: kuwaombea. Kama unavyoamka usiku kumuomba Allah Mtukufu akusaidie katika mambo yako binafsi, basi waombee pia ndugu zetu wa Gaza, kwani maumivu yao ni yetu pia.



**DARASA LA WIKI**

**SEHEMU YA 1**



**SHEIKH**
Seif Ruga
0712 690 811

# Uaminifu, msingi wa jamii bora na maadili mema



**Uaminifu ni miongoni mwa nguzo kuu za maadili ya Uislamu na mojawapo ya majukumu mazito aliyobeba mwanadamu, baada ya mbingu, ardhi na milima kushindwa kuibeba kutokana na uzito wake.**

ربيع أول

NASAHA ZA WIKI 0787 503 085



NA YUSUFU AMINI

# Hukumu inayowasubiri wanaofuja mali za umma

Miongoni mwa taratibu za Mwenyezi Mungu kwa waja ni kwamba ukubwa wa malipo au adhabu hutokana na uzito wa tendo la mhusika. Kanuni ya kisharia inasema: "Aljazaa min jinsil amal" (Malipo ni kwa mujibu wa kitendo).

Hivyo, hata Siku ya Kiyama watu wataingizwa Motoni kulingana na maovu waliyoyafanya. Mwenyezi Mungu anasema: "Kisha kwa yakini tutawatoa katika kila taifa miongoni mwao wale waliomuasi zaidi Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema. Tena hakika sisi tunawajua vilivyo wanaostahiki zaidi kuunguzwa humo." [Qur'an, 19:69–70].

Bila shaka, ubaya na madhara ya ubadhirifu wa mali ya umma ni makubwa mno. Kwa hiyo, marejeo ya wabadhirifu ni mabaya zaidi na adhabu itakayowafika ni kubwa mno.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amebainisha adhabu inayowakumba wabadhirifu wa mali ya umma aliposema: "Hakika watu wanaotumia mali ya Allah (mali ya umma) pasina haki, hao wana Moto Siku ya Kiyama." [Bukhari].

Tunapozungumzia mali ya umma, tunamaanisha mali inayomilikiwa na jamii yote bila kuainishwa kwa watu maalum, na ambayo hutambulika kama hazina ya taifa. Mali hiyo inajumuisha rasilimali zitokanazo na vyanzo mbalimbali, kama vile kodi, huduma zinazotolewa kwa malipo na rasilimali nyingine za umma zinazoliingizia taifa kipato.

Mali hii hutumiwa kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa, na husimamiwa na kulindwa na kiongozi au mtawala, ambaye ana jukumu la kusimamia matumizi yake pamoja na kuhakikisha inatunzwa na kutumika kwa maslahi ya umma.

Kiongozi husaidiwa na timu ya watendaji wa serikali, na kila mmoja hupata ujira wake kutoka katika hazina ya taifa. Miongoni mwa majukumu ya kiongozi ni kusimamia na kutumia mali ya umma iliyo chini ya mamlaka yake kwa uaminifu, akitambua kuwa yeye ni msimamizi tu wa mali hiyo na hana mamlaka ya kuitumia kwa maslahi binafsi.

Akienda kinyume na wajibu huo, atakuwa amefanya khiyana na atakuja na alichokipora Siku ya Hesabu, kama alivyoashiria Mtume (Allah amshushie rehema na amani): "Mtu yeyote tuliyempa kazi miongoni mwenu, na akaficha japo kipande cha uzi au zaidi, atakuwa amefanya khiyana, na atakuja na khiyana yake Siku ya Kiyama." [Muslim].

Ifahamike kuwa Uislamu haukatazi mtu kumiliki mali binafsi, bali unatoa angalizo kuwa wamiliki wataulizwa kuhusu vyanzo vya upatikanaji wa mali hizo na jinsi walivyozitumia.

Mtume amesema: "Nyayo za mja hazitaondoka (Siku ya Kiyama) mpaka aulizwe umri wake aliutumiaje, elimu yake kaifanyia nini, mali yake kaichumaje na kaitumia katika mambo gani, na mwili wake kauchakaza katika mambo gani." [Tirmidhi na Ibn Hibban].

Kwa sababu hiyo, tuna haja ya kukagua njia tunazotumia kuchuma mali, vinginevyo tutapata hasara katika maisha haya ya dunia na Akhera tuendako.

Tumeelezwa katika historia kuwa Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alikuwa akiwafuatilia watu waliokuwa wakijimilikisha mali ya umma na kuwaeleza hatari ya vitendo hivyo pamoja na hatima mbaya inayowakabili.

Sahaba Abii Humaid AbdurRahman bin Sa'ad As–Sa'idiy (Allah awe radhi naye) ameripoti kuwa Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alimtuma Lutbiyah, mmoja wa watu wa kabila la Azdi, akakusanye sadaka.

Aliporejea alisema: "Hii ni (mali) yenu, na hii nimepewa zawadi." Baada ya kusikia hivyo, Mtume alisimama na kupanda juu ya mimbari, akamsifu Mwenyezi Mungu, kisha akasema: 'Ama baada ya utangulizi huu. Mimi ninamtuma mtu miongoni mwenu kwenye kazi miongoni mwa kazi alizonitawalisha Mwenyezi Mungu, halafu anakuja na kusema, 'Hii ni mali yenu nyinyi, na hii nimepewa mimi zawadi.'

Kwanini asiketi kwa baba yake au mama yake ili aletewe zawadi kama ni mkweli? Naapa kwa Mwenyezi Mungu, hachukui yeyote miongoni mwenu kitu pasina haki isipokuwa atakutana na Mwenyezi Mungu Siku ya Kiyama akiwa amebeba mzigo wake.'" [Bukhari na Muslim].

Viongozi na watumishi wengine wa umma wakilizingatia hili, Mwenyezi Mungu atazibariki riziki zao, kwani watakuwa wametimiza wajibu wao na kujipatia chumo zuri na la halali. Mwenyezi Mungu atawapa ujira mwema kwa huduma walizozitoa katika kuihudumia jamii na kuiletea maendeleo.

Ushauri wangu ni kwamba, ikitokea mtu hana sifa za kutimiza jukumu alilokabidhiwa kwa uadilifu na uaminifu, ni vema akajiengua ili asije kuitumbukiza nafsi yake katika ghadhabu za Mwenyezi Mungu.

Afya Pure Drinking water

"Afya"is natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.

WATERCOM LIMITED
P.o. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email:info@watercomtz.com



# Uaminifu, msingi wa jamii bora na maadili mema

Uaminifu ni miongoni mwa nguzo kuu za maadili ya Uislamu na mojawapo ya majukumu mazito aliyobeba mwanadamu, baada ya mbingu, ardhi na milima kushindwa kuibeba kutokana na uzito wake.

Allah Mtukufu anasema: "Kwa hakika Sisi tulikadimisha amana (majukumu) kwa mbingu na ardhi na milima; na vyote hivyo vikakataa kuichukua na vikaogopa. Lakini mwanaadamu akaichukua..." [Qur'an, 33:72].

Uaminifu ni sifa mahsusi ya Mitume wa Allah, kwani kila mmoja wao alikuwa akiwaambia watu wake: "Hakika mimi ni Mtume mwaminifu kwenu." [Qur'an, 26:107]. Mtume Muhammad (rehema na amani zimshukie) alijulikana tangu utotoni kwa uaminifu wake na alipewa lakabu ya "Mkweli, Mwaminifu" – sifa ambazo hata maadui zake walizithibitisha.

Mtume amesema: "Mambo manne yakipatikana kwako, basi usijali yale ambayo utakuwa huna katika dunia: Kuwa mwaminifu, kusema kweli, kuwa na tabia njema, na kula chakula cha halali." [Ahmad].

Katika kusisitiza umuhimu wa uaminifu, Mtume (rehema na amani zimshukie) aliunganisha sifa hiyo na imani na kuisisitiza mara kwa mara katika khutba zake. Anas (Allah amridhie) amesema kuwa, Mtume wa Allah kila alipokuwa akihutubia alisema: "Hana imani yule ambaye si mwaminifu, na hana dini yule ambaye hatekelezi ahadi zake." [Ahmad].

Kadhalika, Imam Qurtubi (Allah amrehemu) amesema: "Uaminifu unahusisha kila jambo analolibeba mwanadamu katika dini yake na dunia yake, kwa kauli na kwa vitendo. Uaminifu ni kutekeleza haki na kuzilinda."

## Aina za uaminifu

Katika Uislamu kuna aina nyingi za uaminifu, miongoni mwa hizo ni uaminifu katika ibada. Muislamu anapaswa kushikamana na faradhi za dini na kuzitekeleza ipasavyo, kuanzia sala, swaumu, zaka, kuwafanyia wema wazazi na faradhi nyingine zote kwa uaminifu.

Mtume amesema: "Atakayehifadhi swala itakuwa nuru, hoja na wokovu kwake Siku ya Kiyama; na asiyeihifadhi hatakuwa na nuru wala hoja wala wokovu..." [Ahmad]. Naye Umar bin Khattwab (Allah amridhie) amesema: "Anayehifadhi swala anaihifadhi dini yake, na anayepuuza swala ni rahisi zaidi kuyapuuza (mambo) mengine."

## Uaminifu katika viungo vya mwili

Viungo vyote vya mwili, kuanzia macho na masikio hadi mikono na miguu ni amana inayopaswa kulindwa. Kwa hiyo, ni wajibu kuvitumia katika mema na kuviepusha na mambo ya haramu.

Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Jicho huzini na moyo huzini; zinaa ya jicho ni kuangalia, na zinaa ya moyo ni kutamani, na tupu huthibitisha (tendo hilo) au hulikataa." [Ahmad].

Ni kwa sababu hiyo, katika tukio la ufunguzi wa mji wa Makka, Mtume alikataa kutumia ishara ya macho kwa hila, akasema: "Haifai kwa Nabii kuwa na hila (kufanya hiyana) ya macho." [Ahmad].

Hii inaonesha kiwango cha juu cha uaminifu na kujiepusha na hiyana hata katika hali ngumu. Hivyo basi, uaminifu ni miongoni mwa misingi mikuu ya Uislamu. Jamii inapozingatia uaminifu hutengemaa; na inapoupoteza, maadili hudidimia na ufisadi huota mizizi.

## Uaminifu katika kuhifadhi mali za watu

Muislamu anatakiwa kuhifadhi mali alizoachiwa na watu na kuzirejesha wanapozihitaji, zikiwa katika hali ileile aliyokabidhiwa. Hivyo ndivyo alivyofanya Mtume wa Allah kwa washirikina na watu wengine waliokuwa wakimwachia amana zao azilinde.

Katika Hadithil Qudsy, Allah amesema: "Watu watatu nitakuwa mgomvi wao Siku ya Kiyama: Mtu aliyetoa ahadi kwa jina langu kisha akaivunja, mtu aliyemuuza mtu huru kisha akala thamani yake, na mtu aliyeajiri mfanyakazi wakakubaliana kisha asimpe ujira wake." [Bukhari].

Nae Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Mwenye kuchukua mali za watu kwa nia ya kuzilipa, Allah atamlipia; na mwenye kuzichukua kwa nia ya kuziharibu, Allah atamwangamiza." [Bukhari].

## Uaminifu katika majukumu

Kila Muislamu anapaswa kutekeleza majukumu yake kwa ubora na uaminifu. Mfanyakazi anapaswa kufanya kazi kwa umakini na uadilifu, kadhalika mwanafunzi anapaswa kujitahidi katika masomo yake. Hii ni kwa sababu kila mtu ana jukumu ambalo ni amana kwake, awe kiongozi, baba, mama au mtoto.

Hivyo, ni wajibu kutunza amana hizo kwa uadilifu, kwa kuzingatia kauli ya Mtume wa Allah: "Kila mmoja wenu ni mchungaji, na kila mmoja ataulizwa kuhusu alichokichunga."

Aidha, miongoni mwa amana kubwa ni kulinda siri za maisha ya ndoa. Mtume amesema: "Hakika miongoni mwa amana kubwa mbele ya Allah Siku ya Kiyama ni mtu kufanya tendo la ndoa na mkewe kisha kuwahadithia watu wengine." [Ahmad].

Kufichua siri za faragha ni hiyana kubwa inayostahiki onyo kali. Hivyo, wanandoa wana wajibu wa kuheshimiana, kusaidiana na kuzingatia haki za kila mmoja, hasa katika nyakati za udhaifu, kama vile maradhi na uzee.




*Itaendelea katika toleo lijalo, Insha Allah*

ربيع أول

# فتاوى



SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Mtume kufunga siku aliyozaliwa, Jtatu, ni hoja ya uhalali wa 'birthday'?

**Swali: Naomba unikinaishe hapa katika kadhia ya sherehe za siku za kuzaliwa watoto kila mwaka (birthday). Je wanaotumia hadith ya mtume kufunga Jumatatu kama kumbukumbu ya mazazi yake wapo sahihi?**

**Jibu:** Hapa kuna kadhia muhimu inayohitaji kutofautisha mambo mawili: hukumu ya kufanya birthday kila mwaka, na hoja inayotolewa kwamba Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alifunga Jumatatu kwa sababu hiyo ndiyo siku aliyozaliwa

## Mosi, usahihi wa hadith

Hadith ya kufunga Jumatatu ni sahihi. Mtume alipoulizwa kuhusu kufunga siku ya Jumatatu, alisema: "Hiyo ni siku niliyozaliwa, na siku niliyotumwa (kuwa Mtume), au siku nilipoteremshiwa wahyi." [Muslim].

Ni sahihi kabisa kusema kwamba Mtume alifunga Jumatatu na miongoni mwa sababu alizotaja ni kwamba hiyo ndiyo siku aliyozaliwa. Lakini je, hadith hii inathibitisha 'birthday' ya kila mwaka? Hapana, si kwa maana hiyo.

Mtume hakusema: "Kwa kuwa hii ni siku yangu ya kuzaliwa, kila mwaka ifanyeni kuwa sikukuu", bali alionesha aina ya ibada aliyofanya: kufunga siku hiyo. Kwa hiyo, kinachothibiti kutoka kwake ni kufunga Jumatatu, si kuanzisha sherehe ya kila mwaka ya kuzaliwa.

Na kuna jambo la kuzingatia sana. Jumatatu inarudi kila wiki, wakati Birthday inayofanywa na watu wengi inakuwa tukio la kila mwaka lenye chakula, keki, zawadi, mikusanyiko na kadhalika. Hivyo si sahihi kuunganisha moja kwa moja mambo hayo mawili kana kwamba Mtume aliweka msingi wa sherehe ya birthday.

## Pili, kwa nini Mtume alitaja siku ya kuzaliwa kwake?

Wanazuoni wameeleza kuwa katika hadith hii kuna kushukuru neema ya Allah kwa ibada.

Mtume alipoulizwa kuhusu kufunga Jumatatu, hakutoa jibu la "sherehe", alitoa jibu la ibada.

Hii inatufundisha kanuni muhimu: Kumshukuru Allah kwa neema ya kuzaliwa au tukio kubwa hakumaanishi kwamba tunaruhusiwa kuunda aina mpya ya ibada au sherehe ambayo Mtume hakufanya. Kwa hiyo mtu akisema: "Mtume alifanya kumbukumbu ya siku yake ya kuzaliwa kwa kufunga Jumatatu, kwa hiyo birthday ni Sunna" si hoja sahihi. Kilichothibiti ni kufunga Jumatatu, na si kwamba Mtume alikuwa akiadhimisha "birthday" kwa maana inayofanywa leo.

## Tatu, vipi kuhusu birthday za watoto?

Hapa ndipo ningependekeza usichanganye hukumu ya birthday na furaha halali ya mtoto. Mzazi anaweza kumfurahisha mtoto wake, kumpa zawadi, kumlisha chakula kizuri, kumwombea dua, kumpongeza kwa mafanikio yake, n.k. Haya hayahitaji kuitwa birthday wala kufanywa kuwa ibada.

Lakini kuifanya siku ya kuzaliwa kuwa sherehe maalumu inayorudiwa kila mwaka, ndipo suala la kisheria linapokuja. Kwa mtazamo wa Sunna na misingi ya ibada, hoja ya kufunga Jumatatu haiwezi kutumika kuhalalisha sherehe hiyo.

## Nne, Jibu fupi kabisa la hoja hii

Mtu akikuambia: "Mtume alifunga Jumatatu kwa sababu ndiyo siku aliyozaliwa, kwa hiyo birthday ni halali." Unaweza kumjibu: "Ni kweli Mtume alisema kwamba Jumatatu ni siku aliyozaliwa na kwa sababu hiyo alikuwa akifunga.


Lakini Sunna aliyoiweka ni kufunga Jumatatu, si kuifanya siku ya kuzaliwa kuwa sherehe ya kila mwaka.

Kwa hiyo hadith inathibitisha kufunga Jumatatu, lakini yenyewe haithibitishi birthday." Na kuna tofauti kubwa kati ya "kukumbuka neema kwa ibada iliyothibiti" na "kuanzisha sherehe maalumu kwa ajili ya kumbukumbu hiyo." Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

ربيع أول

Na Zaharani Baraka
018 424 258

# Adabu za vikao vya faragha katika Uislamu



Uislamu ni dini ya maumbile ambayo mafundisho yake yanaangazia nyanja zote za maisha ya mwanadamu. Si dini ya kiroho na imani pekee, bali ina mfumo wa maisha unaomwelekeza muumini kuwa mtiifu kwa Muumba wake katika kila hatua ya maisha, tangu anapoamka hadi anaporejea kitandani.

Miongoni mwa mafundisho muhimu ya Uislamu ni kushikamana na tabia na mwenendo mwema, ambao ni msingi wa kujenga jamii yenye mshikamano, upendo na kuheshimiana. Katika muktadha huo, Uislamu umeweka nidhamu kuhusu mazungumzo ya faragha au minong'ono, hususan pale yanapotumika kupanga mambo yanayoweza kuwadhuru wengine.

Mazungumzo ya siri ni hali ya watu wawili au zaidi kukaa pamoja na kupanga, kushauriana au kuweka mikakati bila kutaka wengine wajue wanachozungumza. Ingawa si kila mazungumzo ya faragha ni mabaya, mengi yanaweza kukosa manufaa au kutumiwa kupanga uovu, ikiwemo kuwadhuru watu wengine.

Qur'an inasema: "Hakuna kheri katika mengi wanayoshauriana kwa siri, isipokuwa anayesema sadaka au kufanya wema au kupatanisha baina ya watu. Na atakayefanya hayo kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu, tutampa ujira mkubwa." [Qur'an, 4:114].

Aya hii inafahamisha kuwa mazungumzo ya siri yanapaswa kuwa na lengo jema. Badala ya kutumia vikao hivyo kwa porojo, kusengenya, kueneza umbea au kupanga mambo ya haramu, Waislamu wanahimizwa kuvitumia kwa kuamrishana mema, kusaidiana na kupatanisha waliogombana.

## Hakuna siri mbele ya Allah

Mwanadamu anaweza kuwaficha watu kile anachokizungumza kwa siri, lakini hawezi kumficha Mwenyezi Mungu. Qur'an inasema: "Je, huoni kwamba Mwenyezi Mungu anajua vilivyomo mbinguni na ardhini? Haupatikani mnong'ono wa watatu ila Yeye huwa wa nne wao, wala wa watano ila Yeye huwa wa sita wao..." [Qur'an, 58:7].

Kwa hiyo, muumini anayemcha Mwenyezi Mungu hawezi kujisikia huru kupanga uovu akiwa faraghani. Anaamini kwamba Mwenyezi Mungu anajua kila analolizungumza na kila analolipanga, na kwamba matendo yake yote yatahesabiwa Siku ya Kiyama.

Qur'an pia inawaonya waumini dhidi ya kutumia mazungumzo ya siri katika dhambi na uadui: "Enyi mliyoamini! Mnaponong'ona, msinong'one juu ya mambo ya dhambi na uadui na kumuasi Mtume, bali zungumzeni juu ya wema na uchamungu." [Qur'an, 58:9].

Mafundisho haya yanaonesha kwamba minong'ono inayolenga kuwahuzunisha au kuwadhuru waumini ni jambo linalopaswa kuepukwa. Qur'an inaeleza kuwa mazungumzo hayo mabaya yanatokana na shetani ili kuwahuzunisha walioamini, ingawa hayawezi kuwadhuru bila idhini ya Mwenyezi Mungu. [Qur'an, 58:10].

## Nidhamu katika vikao vya faragha

Mtume (rehema na amani za Mwenyezi Mungu zimshukie) amesema: "Mkiwa watatu, basi wawili wasinong'one bila ya kumshirikisha wa tatu mpaka mchanganyike na watu wengine, isije kumhuzunisha." [Muslim].

Hadith hii inafundisha umuhimu wa kuzingatia hisia za wengine. Mazungumzo ya siri mbele ya mtu mwingine yanaweza kumfanya ajihisi ametengwa, kudharauliwa au kuzungumziwa vibaya.

Kwa msingi huo, Waislamu wanapaswa kutumia vikao vyao vya faragha kwa mambo yenye kheri, kama kuamrishana mema, kukatazana maovu, kusaidiana, kutatua migogoro na kuimarisha udugu.

Vikao hivyo pia vinaweza kutumika kumtaja Mwenyezi Mungu na kumswalia Mtume. Uislamu haukatazi kila mazungumzo ya siri, bali umeweka mipaka na kuhimiza yatumiwe kwa lengo jema.

Mazungumzo yanapogeuka kuwa chombo cha kupanga dhuluma, uadui au kuwahuzunisha wengine, hugeuka kuwa chanzo cha madhara katika jamii. Muumini anapaswa kukumbuka kwamba hata siri kubwa inayofichwa na wanadamu iko wazi mbele ya Mwenyezi Mungu.

Na Abeid Othman
0754 990 083

# Hii ndio sababu ya Waislamu wengi kukwepa zaka

Zaka ni miongoni mwa nguzo kuu za Uislamu na imepewa nafasi kubwa sana katika Qur'an na Sunna.

Mara nyingi Qur'an inapozungumzia swala, inaambatanisha pia na zaka. Allah anasema: "Na simamisheni Swala na toeni Zaka." [Qur'an 2:43].

Hili linaonesha wazi kwamba zaka si jambo la hiari au sadaka ya kawaida ambayo Muislamu anatoa anapojisikia, bali ni ibada yenye masharti yake ambayo imefaradhishwa kwa mwenye mali inayofikia kiwango kilichowekwa na Sharia.

Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) naye amesema: "Zaka inachukuliwa kutoka katika mali ya watu na kurejeshwa kwa mafukara wao." Kwa hiyo, zaka ina nafasi mbili kubwa: ni ibada kati ya mja na Allah, na wakati huo huo ni mfumo wa kijamii wa kuwasaidia wenye uhitaji.

Lakini swali kubwa tunalopaswa kujiuliza leo ni hili: Kwa nini Waislamu wengi hawatoi zaka, licha ya kuwa ni nguzo ya Uislamu?

Moja ya sababu kubwa ni namna ambavyo tumefundishwa kuhusu zaka katika mifumo yetu ya elimu ya dini, hasa katika baadhi ya madrasa. Wengi wamezoeshwa kuelewa kwamba zaka ni jambo la matajiri pekee. Hapa ndipo tatizo lilipo.

Kauli ya jumla kwamba "zaka ni ya matajiri" inaweza kumfanya mtu mwenye mali inayofikia nisabu ajione hana wajibu wa kutoa zaka kwa sababu tu hajioni kuwa ni tajiri.

Ukweli wa msingi ni kwamba wajibu wa zaka haujengwi juu ya mtu kujitambulisha kuwa tajiri au maskini; unajengwa juu ya aina ya mali, kufikia nisabu na masharti mengine yaliyowekwa na Sharia.

Nisabu ni kiwango cha chini ambacho mali inapofikia ndipo inakuwa katika kiwango kinachoweza kuwajibisha zaka.

Kwa mfano, mtu anaweza kuwa hana nyumba kubwa, gari la kifahari au maisha yanayoonekana ya kitajiri, lakini akawa na fedha au mali nyingine inayofikia nisabu. Mtu huyo hawezi kusema, "Mimi si tajiri, kwa hiyo sitoi zaka."

Kinachotakiwa kuangaliwa ni kama mali yake imefikia kiwango kinachowajibisha zaka na kama masharti yake yametimia.

## Zaka si ya fedha pekee

Tatizo lingine ni kufikiri kwamba zaka inahusu fedha taslimu pekee. Sharia imeweka aina mbalimbali za mali zinazoweza kuwa na zaka, zikiwemo dhahabu na fedha, bidhaa za biashara, mifugo na mazao ya kilimo, huku kila aina ikiwa na masharti na viwango vyake.

Hii ina maana kwamba Muislamu anayelima na kuvuna mazao ana wajibu wa kujifunza hukumu ya zaka ya mazao yake.

Zaka ya mazao pia ina tofauti na zaka ya fedha; kwa mfano, katika mfumo unaotajwa katika vyanzo vya fiqhi, mazao yanayomwagiliwa kwa mvua au maji ya asili yana kiwango tofauti na yale yanayohitaji gharama za umwagiliaji.

Vivyo hivyo, wafugaji nao wanapaswa kujifunza hukumu za zaka ya mifugo. Mtume alitoa maelekezo kuhusu nisabu ya mifugo, na Hadith inaonyesha uzito wa kutotoa zaka ya mifugo pale inapowajibika. Tanzania ni nchi ambayo watu wengi wanajishughulisha na kilimo na ufugaji. Lakini bado kuna dhana kwamba mtu anayelima au kufuga ni lazima awe "tajiri mkubwa" ndipo afikiri kuhusu zaka.

## Hii si sahihi kama msingi wa jumla.

Mkulima anaweza kuwa na mavuno yanayofikia masharti ya zaka lakini akasema, "Mimi sina utajiri, ni mkulima tu." Mfugaji anaweza kuwa na mifugo inayofikia nisabu lakini akasema, "Hii ni mifugo yangu ya kawaida, mimi si tajiri." Tatizo hapa si mali pekee, bali ni uelewa wa hukumu ya zaka.

Ndiyo maana elimu ya zaka inapaswa kutolewa kwa lugha inayoeleweka na kwa mifano ya maisha halisi ya Watanzania.

Mkulima ajue zaka ya mazao yake. Mfugaji ajue zaka ya mifugo yake. Mfanyabiashara ajue zaka ya mali ya biashara. Mwenye fedha ajue zaka ya fedha. Na mwenye dhahabu ajue hukumu ya dhahabu yake.

## Wafanyabiashara msijizubaishe

Katika jamii yetu wapo wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa. Baadhi yao wana mali nyingi katika biashara lakini hawatoi zaka kwa sababu wanajiona bado hawajawa "matajiri."

Wanazuoni wengi wameeleza kuwa bidhaa za biashara ni miongoni mwa mali zinazowajibisha zaka, kwa kutegemea masharti yake.

Ushahidi umetolewa pia kwa kauli ya Samurah bin Jundub kwamba Mtume (Rehma na amani zimshukie) alikuwa akiwaamuru Maswahaba kutoa zaka katika mali walizokuwa wameziandaa kwa ajili ya kuuza.

Kwa hiyo, mfanyabiashara hapaswi kuangalia tu kiasi cha pesa kilicho mfukoni mwake. Anapaswa kujifunza namna ya kuhesabu mali ya biashara inayohusika na zaka kwa mujibu wa masharti ya Sharia.

Jambo jingine linalohitaji elimu zaidi ni dhahabu zinazomilikiwa na wanawake. Katika jamii zetu kuna wanawake wenye mikufu, bangili, pete, hereni na mapambo mengine ya dhahabu yenye thamani kubwa.

Baadhi ya dhahabu hizo zinaweza kufikia nisabu, lakini suala la zaka yake limeachwa kwa sababu ya kutokuwepo kwa elimu ya kutosha au kutokana na tofauti za kifiqhi kuhusu baadhi ya aina za mapambo yanayotumika.

Kwa hiyo, badala ya kusema moja kwa moja kwamba "dhahabu ya mwanamke haina zaka" au "zaka ni ya matajiri," ni muhimu mtu kujifunza hukumu inayohusika kulingana na aina ya dhahabu, kiwango chake, matumizi yake na madhehebu/wanazuoni anaowafuata. Dhahabu na fedha zimetajwa miongoni mwa mali zinazohusika na zaka zinapofikia nisabu na kutimia masharti yake.

## Tubadili elimu kuhusu zaka

Hapa ndipo tunapopaswa kufanya tathmini kubwa. Kama madrasa zetu zinawafundisha watoto na vijana kwamba zaka ni "ya matajiri" bila kuwafundisha kwa kina maana ya nisabu, aina za mali, masharti na namna ya kuhesabu zaka, tunawaacha na uelewa usiokamilika.

Mtoto anayefundishwa zaka anapaswa kuambiwa: Zaka si kwa mtu anayejiona tajiri; zaka ni kwa mali inayofikia masharti yaliyowekwa na Sharia.

Na Said Rajab
0783 650 803

# Maisha na urithi wa Mtume Muhammad


## SEHEMU YA 1

**Wakati wa kuikomboa Makka, Mtume Muhammad (rehema za Allah na amani zimshukie) alikuwa na umri wa takriban miaka 60, akichukuliwa kuwa mtu mzima kwa viwango vya wakati huo.**

**Misingi ya imani ya Uislamu ilijengwa katika jamii kupitia mafundisho yake na ufunuo wa Qur'an Tukufu uliokuwa ukiendelea kushuka. Misingi hiyo ilijumuisha ibada na desturi za kidini, kanuni za kijamii, pamoja na misingi ya utawala wa Kiislamu.**

**Mpangilio mpya wa kijamii uliibuka, ukavuka mipaka ya ukabila na utaifa na kujenga jamii moja ya Kiislamu iliyoongozwa na sharia ya Mwenyezi Mungu.**

**Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) alisisitiza dhana hiyo katika khutba yake ya mwisho, akieleza kuwa asili ya wanadamu wote inatokana na Adam. Alisisitiza pia kuwa uchamungu ndiyo msingi mkuu unaowatofautisha watu.**



### Himaya iliyounganishwa kipekee

Ujumbe wa Mtume ulijumuisha pia kipengele cha siasa kilichosaidia kuunda himaya ya kwanza iliyoungana ya Waislamu katika Rasi ya Arabuni. Muungano huo wa makabila ya Kiarabu haukuwa jambo la kawaida katika historia ya eneo hilo.

Mtume aliwafikia pia watu wa maeneo yaliyopakana na himaya za Warumi na Uajemi. Hatua hiyo haingeweza kupuuzwa na majirani hao wenye nguvu, ambao baadaye walilazimika kulichukulia kwa uzito suala la kuenea kwa Uislamu kwa kasi.

### Kujiandaa kwa mustakabali wa umma

Baada ya kuikomboa Makka, Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) alirejea Madina, ambako aliendelea kuongoza umma wa Waislamu. Hatua hiyo ilikuwa sehemu ya kutekeleza makubaliano aliyokuwa amefanya na makabila ya Aus na Khazraj miaka kadhaa iliyotangulia.

Mkazo wake ulielekezwa pia katika kuhakikisha ustawi na mustakabali wa umma baada ya kifo chake. Mtume aliwasisitiza waumini kutekeleza wajibu wao ipasavyo, kuhifadhi Qur'an na kufuata Sunna yake.

### Hijja ya kuaga na ujumbe wa usawa

Mwaka 632 Miladia, Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) alifanya Hijja yake ya mwisho mjini Makka. Akihutubia maelfu ya wafuasi wake waliovalia mavazi meupe, akiwaweka katika hali ya usawa bila kujali utajiri wala hadhi zao, Mtume aliwakumbusha kuhusu utu na ubinadamu wao.

Aliwasihi waepuke ukandamizaji, wawaheshimu na kuwathamini wanawake, na waachane na ushindani wa kikabila ambao ulikuwa umeigawa jamii ya Kiarabu kwa karne nyingi.

Hotuba hiyo ya kuaga ilijumuisha maelekezo mbalimbali kuhusu maisha ya mtu binafsi na jamii kwa ujumla, huku ikisisitiza mabadiliko makubwa katika nyanja mbalimbali za maisha. Wafuasi wake waliiona kama msingi wa mpangilio mpya wa jamii unaotegemea sharia ya Mwenyezi Mungu na mafundisho ya Utume wake.

### Kuweka misingi ya upanuzi

Baada ya kumaliza Hijja, Mtume alirejea Madina na kuendelea na juhudi za kuueneza Uislamu. Wanazuoni na walimu walitumwa katika jamii mpya zilizosilimu katika maeneo mbalimbali ili kuwafundisha misingi ya Uislamu.

Madina, ikiwa kituo cha karibu zaidi na Mtume iliendelea kuwa kitovu cha maarifa ya Kiislamu na kuwa na nafasi muhimu katika kuielimisha jamii ya Waislamu hata baada ya kifo chake.

Msafara wa kijeshi pia uliandaliwa kuelekea upande wa Himaya ya Warumi. Katika maandalizi hayo, Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) alisisitiza maadili na kanuni za Kiislamu ambazo zingekuwa mwongozo wa majeshi ya Waislamu katika vipindi vilivyofuata.

*Itaendelea wiki ijayo, Insha Allah*

ربيع أوّل

MAKALA MAALUM

Na Said Rajab
0783 650 803

# Mchango wa Uislamu katika teknolojia ya AI

## SEHEMU YA 3

**Tunaendelea kuangazia mchango wa wanasayansi wa Kiislamu walioishi katika Zama za Dhahabu za Uislamu, ambao waliweka misingi ya maarifa yaliyokuja kutumika baadaye katika teknolojia ya Akili Unde (AI) tunayoiona leo.**

**Katika makala ya leo, tunamwangazia mwanafalsafa na mwanazuoni wa Kiislamu, Abu Ali al–Husayn Ibn Abd Allah Ibn Sina, anayejulikana zaidi kama Ibn Sina na katika ulimwengu wa Magharibi kama Avicenna.**

Ibn Sina aliishi kati ya mwaka 980 na 1037 BK na alikuwa miongoni mwa wanazuoni wa mwanzo kuchunguza kwa kina namna michakato ya utambuzi wa binadamu inavyoweza kuigwa. Maarifa hayo yalikuja kuwa na umuhimu katika maendeleo ya baadaye ya teknolojia ya AI.

Aidha, Ibn Sina alichunguza asili ya fahamu na kujitambua kwa kutumia majaribio ya kimawazo, likiwamo jaribio maarufu linalojulikana kama "Floating man", yaani "Mtu anayeelea" au "Mtu aliyesimamishwa hewani."

Katika hoja yake, Ibn Sina alidai kuwa ufahamu unaweza kuwepo kwa kujitegemea bila kutegemea taarifa kutoka kwenye milango ya fahamu (sensory input). Dhana hii bado inajadiliwa katika falsafa ya akili, sayansi ya utambuzi na maadili ya teknolojia ya Akili Unde.

Sensory input ni ishara au taarifa yoyote inayotoka katika mazingira au mwilini na kupokelewa na viungo vya fahamu. Uchunguzi wa Ibn Sina kuhusu utambuzi, kumbukumbu na 'reasoning' uliwakilisha hatua muhimu katika jitihada za kuelewa na kuiga namna binadamu anavyofikiri.

'Reasoning' ni mchakato wa kiakili wa kutumia maarifa, ukweli na mantiki kuchambua taarifa, kutatua matatizo na kufikia hitimisho.

Mawazo ya Ibn Sina yanaonekana pia katika utafiti wa kisasa wa AI, hususan katika eneo la usanifu wa utambuzi (cognitive architecture) – mifumo iliyoundwa kuiga namna binadamu anavyofikiri, kujifunza na kufanya maamuzi.

### Badi al–Zaman al–Jazari

Mwanasayansi mwingine kutoka katika ulimwengu wa Kiislamu ni Badi al–Zaman al–Jazari, aliyeishi kuanzia mwaka 1136 hadi 1206 BK. al–Jazari alikuwa mhandisi aliyebobea katika kubuni mashine za kiotomatiki na mifumo iliyokuwa na uwezo wa kutekeleza maagizo yaliyopangwa.

Mchango wake unaweza kueleweka vizuri kupitia dhana mbili zinazotumika katika teknolojia ya kisasa: Programmable Machines na Embodied AI. Programmable Machine ni kifaa kinachoweza kuhifadhi, kubadilisha na kutekeleza seti ya maagizo au msimbo (code) kwa ajili ya kufanya kazi maalumu.

Ama Embodied AI, ni aina ya Akili Unde inayounganishwa katika mwili au mfumo halisi na hivyo kuiwezesha kutambua mazingira, kujifunza na kuingiliana moja kwa moja na ulimwengu halisi.

al–Jazari alibuni baadhi ya vifaa vya kiotomatiki vya mwanzo kabisa duniani. Mitambo yake iliweza kutekeleza kazi mbalimbali kwa kiwango fulani cha kujitegemea bila kuhitaji uingiliaji wa moja kwa moja wa binadamu katika kila hatua.

### Mwendelezo wa maarifa na kuunganisha nukta


Michango ya pamoja ya al–Khwarizmi, al–Kindi, Ibn Sina na al–Jazari iliunda mkondo mpana wa maarifa uliounganisha hisabati, mantiki, falsafa na uhandisi – taaluma ambazo zimeendelea kuwa muhimu katika maendeleo ya teknolojia ya AI hadi leo.

Kazi zao ziliweka misingi ya baadhi ya vipengele muhimu vinavyohusishwa na Akili Unde, muda mrefu kabla ya kuibuka kwa kompyuta za kidijitali.

Wanazuoni hao walichukulia maarifa hayo kuwa amana yenye hadhi kubwa, iliyopaswa kutumiwa kwa manufaa ya mwanadamu. Mtazamo huo wa kimaadili una uhusiano wa karibu na mijadala ya kisasa kuhusu maadili katika matumizi ya AI, ikiwemo masuala ya haki, upendeleo, uwazi na athari zake kwa jamii.

Pia walisisitiza umuhimu wa nia njema na uwajibikaji katika matumizi ya maarifa. Kanuni hizo zinaendelea kuwa muhimu katika dunia ya leo, ambapo mifumo ya teknolojia ya AI inazidi kuwa na uwezo mkubwa na kuenea katika nyanja mbalimbali za maisha.

*Itaendelea wiki ijayo Insha Allah*



**John McCarthy baba wa akili bandia (Artificial Intelligence - AI). Yeye ndiye aliyebuni neno "Artificial Intelligence" na kuweka misingi ya tawi hili la sayansi mwaka 1956.**

# TAFAKURI YA WIKI

NA SAMRATH MSUYA
0789 201 383




# Ndugu, jamaa na marafiki kama 'bima' ya kijamii

MWEZI mmoja uliopita, rafiki yangu mmoja alipata mtihani wa maradhi makubwa akalazwa Muhimbili, lakini siku ambayo alifanyiwa upasuaji, mkewe akapata ajali akiwa njiani kumuangalia mumewe. Alivunjika mguu, akalazwa Moi. Akiwa hana ndugu yoyote, marafiki zake tuliwasitiri mpaka walipopona.

Wiki hii nikashuhudia janga jingine lililomkumba ndugu yangu aliyepoteza karibu kila kitu baada ya nyumba aliyokuwa amepanga kuteketea kwa moto. Kwa mara nyingine, Makundi ya WhatsApp yakatumika kusambaza taarifa. Ndugu na jamaa wakaambiwa na kuhimizwa kusaidia kwa kadiri ya uwezo wao.

Lakini kati ya matukio haya mawili niliona tofauti kubwa.

Yule rafiki yangu aliyeugua na mkewe, alikuwa mtu wa watu. Alishirikiana nao, alizungumza nao, alihudhuria mambo yao  na lilipomkumba tatizo alikimbiliwa haraka

Haikuwa hivyo sana kwa ndugu yetu aliyepatwa na janga la moto. Kwa muda mrefu alijitenga na kuishi maisha yake mwenyewe. Hakushiriki sana katika misiba, harusi au shughuli nyingine za kijamii.

Alisahau kuwa ndugu, jamaa, majirani na marafiki ni aina fulani ya kinga ya majanga, sio kama mkataba wa  takaful bali mwitikiao wa ule mtandao wa watu ambao, janga linapotokea ghafla, hukusimamia kabla hata hujajua utaanzia wapi.

## Binadamu hakuumbwa kuishi peke yake

Katika maisha ya leo, hasa mijini, tunazidi kujifunza kuishi kivyetu. Tunafunga mlango, hatujui hata jina la Jirani yetu.

Tunajitetea: "Mimi sipendi mambo ya watu", lakini kuna tofauti kubwa kati ya kutokuingilia mambo ya watu na kujitenga na watu. Uislamu haujengi jamii ya watu wanaoishi kama visiwa. Unasisitiza undugu, ujirani, kusaidiana na kuhurumiana.

Allah anasema: "Na saidianeni katika wema na uchamungu. [Qur'an, 5:2]. Mahali pengine Qur'an inatuonya kuhusu kuvunja mafungamano ya undugu na kutukumbusha kumcha Allah ambaye kupitia Kwake tunaombana haki pamoja na kuheshimu uhusiano wa jamaa. [Qur'an, 4:1).

Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) naye amefananisha Waumini kwa picha nzuri sana: Muumini kwa Muumini mwenzake ni kama jengo, sehemu moja ikiimarisha nyingine. Kisha akaunganisha vidole vyake kuonyesha namna sehemu hizo zinavyoshikamana. [Bukhari na Muslim].

Huo ndio msingi wa jamii.

## Leo ni kwake, kesho inaweza kuwa kwako

Tunapokwenda kumfariji aliyefiwa, kumtembelea mgonjwa, kuhudhuria harusi, kumjulia hali jirani au kumchangia mwenye janga, mara nyingine tunaweza kuona kama tunampunguzia shida yeye tu.

Lakini kwa namna nyingine tunajenga jamii ambayo nasi tunaishi ndani yake.

Leo unachangia matibabu ya mwenzako. Kesho kwako; leo nyumba ya jirani imeungua. Kesho mafuriko, moto, ajali au tukio jingine linaweza kugonga mlango wako. Hakuna anayepanga majanga.

Ndiyo maana jamii yenye mshikamano ina thamani ambayo haiwezi kupimwa kwa fedha pekee.

Katika lugha ya taaluma, tunaweza kuiita mtaji wa kijamii — yaani thamani inayotokana na mahusiano, kuaminiana na mitandao ya watu. Lakini kwa lugha yetu ya kawaida, ni kuwa na watu.

Na kwa wengi wetu wenye kipato cha kawaida, watu hao ndio huwa msaada wa kwanza wakati mambo yanapoharibika.

Ni bima ya watu wa kawaida.

## Lakini tusifanye urafiki wa maslahi

Hoja yangu si kwamba tuwahudumie watu leo ili kesho watuhudumie. Ukifanya hivyo, undugu unakuwa biashara. Muislamu anamtembelea mgonjwa, anafariji mwenye msiba, anamjali jirani na anasaidia mwenye shida kwanza kwa kutafuta radhi za Allah na kutekeleza wajibu wa kibinadamu.

Lakini moja ya matunda ya jamii inayofanya hivyo ni kwamba watu hawabaki peke yao wakati wa maafa.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesisitiza pia umuhimu wa kuunga undugu. Katika hadith iliyopokewa na Bukhari na Muslim, mafungamano ya jamaa yamepewa nafasi kubwa katika maisha ya Muumini.

Kwa hiyo, faida tunayopata katika mahusiano mema si sababu pekee ya kuyajenga. Ni moja ya matunda yake.

## Usisubiri janga ndiyo uanze kutafuta watu

Maisha ya kijamii yanahitaji uwekezaji.

Mjulie hali ndugu yako. Msalimie jirani. Fika kwenye msiba unapoweza. Mtembelee mgonjwa. Changia jambo la mwenzako kadiri ya uwezo wako. Usione kila mwaliko wa harusi, dua, mazishi au jambo la kifamilia kama usumbufu usio na maana.

Huhitaji kuwa kila mahali. Wala si lazima uwe mtu wa sherehe zote lakini usijenge maisha ambayo hakuna anayekujua, hakuna unayemjua na hakuna anayejua namna ya kukufikia isipokuwa unapokuwa na shida.

Bima nzuri hununuliwa kabla ya ajali, si baada ya ajali. Na kwa maana hiyo, baadhi ya bima muhimu zaidi za maisha hazina karatasi wala malipo ya kila mwezi. Ni ndugu uliowaunga. Ni jirani uliyesalimiana naye. Ni rafiki uliyemsimamia. Ni mgonjwa uliyemtembelea. Ni mwenye msiba uliyemfariji. Ni mtu aliyepata shida ambaye hukupita pembeni kana kwamba humjui.

Kwa sababu siku moja, bila taarifa, maisha yanaweza kukugeuzia upande mwingine. Na wakati huo unaweza kugundua kwamba katika mali zote ulizowahi kukusanya, watu uliokuwa nao vizuri ndio waliokuwa utajiri wako mkubwa zaidi.

NA SAMRATH MSUYA
0789 201 383

# Maneno 9 epuka kuyatamka kazini

**Mahali pa kazi, uwezo pekee hautoshi. Unaweza kuwa mchapakazi, mwenye elimu nzuri na mwenye mawazo bora, lakini namna unavyowasiliana na wengine inaweza kujenga au kuharibu taswira yako kitaaluma.**
**Wakati mwingine tatizo si kile tunachomaanisha, bali namna tunavyokisema. Sentensi moja inaweza kukufanya uonekane mkorofi, hata kama hilo halikuwa kusudi lako. Haya ni maneno na kauli 10 unazopaswa kuzitumia kwa tahadhari kazini.**

### "Umekosea"

Kutofautiana kwa mawazo ni jambo la kawaida kazini. Tatizo huanza pale tunapofanya mjadala wa hoja kuwa mashindano ya nani yuko sahihi.

Kumwambia mwenzako moja kwa moja, "Umekosea," kunaweza kumweka katika hali ya kujitetea. Badala ya kujadili hoja, mjadala unaweza kugeuka kuwa mgongano wa watu.

Ni bora kusema: "Nina wazo jingine ambalo linaweza kutusaidia." Hujaficha msimamo wako, lakini umefungua mlango wa majadiliano.

### "Nilidhani mtu mwingine angefanya"

Hii ni mojawapo ya sentensi zinazoweza kuharibu taswira yako ya uwajibikaji. Inaonyesha kwamba jukumu halikufuatiliwa na sasa lawama zinahamishiwa kwa mtu mwingine.

Badala yake, kubali sehemu yako. Sema: "Nilipaswa kuthibitisha mapema nani alikuwa anawajibika." Uwajibikaji hujenga uaminifu kuliko kutafuta mtu wa kulaumiwa.

### "Siwezi kufanya kazi na mtu huyo"

Ofisini hutachagua kila wakati watu unaotaka kufanya nao kazi. Kutakuwa na tofauti za hulka, mitazamo na mbinu za kufanya kazi.

Ukisema huwezi kufanya kazi na mtu fulani, unaweza kuonekana kama mtu asiyeweza kuendana na mazingira tofauti.

Badala yake uliza: "Tunawezaje kuboresha namna tunavyoshirikiana?" Hapo unahamisha mjadala kutoka kwa mtu kwenda kwenye suluhisho.

### "Ulipaswa kufanya..."

"Ulipaswa kuniambia mapema." "Ulipaswa kujua." "Ulipaswa kuwasilisha jana."

Maneno haya mara nyingi huangalia kosa lililotokea kuliko namna ya kulizuia lisijirudie.

Kazini, hasa panapohitajika ushirikiano, lugha inayotafuta suluhisho huwa na tija zaidi.

Sema: "Wakati mwingine tafadhali nijulishe mapema," au "Tuhakikishe tunapanga hili mapema zaidi."

### "Tumekuwa tukifanya hivi siku zote"

Hii ndiyo sentensi maarufu ya kupinga mabadiliko. Inawezekana kabisa mfumo wa zamani unafanya kazi vizuri. Lakini kusema tu, "Tumekuwa tukifanya hivi siku zote," kunaweza kukufanya uonekane umefungwa na mazoea.

Badala yake uliza: "Njia hii mpya itatupa faida gani?" Hapo unatathmini mabadiliko badala ya kuyakataa bila kuyachunguza.

### "Labda nimekosea, lakini..." au "Huenda hili ni wazo la kijinga..."

Usiliue wazo lako kabla wengine hawajalisikia. Watu wengi hutumia sentensi hizi kujikinga dhidi ya kukosolewa. Lakini mara nyingi matokeo yake ni kudhoofisha ujumbe wao wenyewe.

Kama una hoja, iwasilishe kwa utulivu na kujiamini. Badala ya kusema, "Huenda hili ni wazo la kijinga," sema: "Ninapendekeza tujaribu njia hii." Wazo lako bado linaweza kupingwa, lakini angalau umelipa nafasi ya kusikilizwa.

### "Hii si haki"

Huenda kweli hali si ya haki. Labda umepewa kazi nyingi kuliko wengine, umepitwa kwenye nafasi ya kupandishwa cheo au unaona mgawanyo wa majukumu hauna uwiano.

Lakini kulalamika kwa kusema tu, "Hii si haki," hakuelezi tatizo wala suluhisho. Ni bora kuzungumza na msimamizi wako kwa ushahidi: eleza mzigo wa kazi, matarajio na kile unachoomba kibadilike. Tofautisha kati ya kulalamika na kuwasilisha hoja.

### "Hilo haliwezekani"

Kabla hujasema jambo haliwezekani, jiulize: Haliwezekani kabisa, au ni gumu tu? Waajiri wengi huthamini wafanyakazi wanaoweza kuona changamoto na bado wakatafuta njia.

Badala ya kufunga mjadala kwa kusema, "Haiwezekani," sema: "Hebu tuangalie njia zinazowezekana." Huenda jibu likabaki kuwa hapana, lakini litakuwa jibu lililofikiwa baada ya kuchunguza uwezekano.

### "Nitajaribu"

Kwa lugha ya kawaida, "nitajaribu" inaweza kuonekana kuwa kauli nzuri. Kazini, hata hivyo, inaweza kuacha sintofahamu: Utafanya au hutafanya?

Ikiwa unaona muda au rasilimali ni changamoto, eleza hilo moja kwa moja.

Sema: "Nitahitaji msaada kidogo ili kukamilisha ndani ya muda, lakini nitahakikisha kazi inafanyika."

Hiyo ni ahadi yenye uhalisia kuliko "nitajaribu."

### Maneno hujenga taswira yako

Mawasiliano ya kitaaluma hayamaanishi kujifanya au kuogopa kusema ukweli. Yanamaanisha kujua namna ya kusema ukweli bila kufunga milango ya ushirikiano.

Mara nyingi tofauti kati ya mfanyakazi anayeonekana mgumu na yule anayeonekana mkomavu si hoja wanayotoa. Ni namna wanavyoitoa.

Kabla hujasema jambo kazini, jiulize swali moja rahisi: Je, maneno yangu yanasaidia kutatua tatizo, au yanaongeza tatizo jingine?

Jibu la swali hilo linaweza kubadili kabisa namna watu wanavyokuona kazini.

Na Samrath Msuya
0789 201 383

# Uongozi wa kisasa: Data kabla ya maamuzi

**ZAMANI, uzoefu, mamlaka na uwezo wa kufanya maamuzi ya haraka vilitosha kumjenga kiongozi mwenye nguvu. Kiongozi alisema, "Kwa uzoefu wangu, tufanye hivi," na mara nyingi uamuzi uliishia hapo.**

**Sifa hizo bado zina umuhimu. Lakini katika dunia ya leo, hazitoshi peke yake. Mashirika, kampuni, shule, taasisi na hata biashara ndogo zinazalisha taarifa nyingi kila siku: mauzo, gharama, mahudhurio, malalamiko ya wateja, utendaji wa wafanyakazi, matumizi ya huduma, mitazamo ya wateja na mwenendo wa soko.**

**Swali sasa si kama taarifa hizo zipo. Swali ni: Kiongozi anazitumiaje kufanya maamuzi?**

**Hapo ndipo dhana ya data-driven decision-making inapoingia — yaani kufanya maamuzi kwa kutumia ushahidi unaotokana na taarifa badala ya kutegemea hisia, mazoea au makisio pekee.**

## Data haisemi "acha kutumia akili"

Uongozi unaotumia data haumaanishi kiongozi anakuwa mtumwa wa namba.

Badala yake, data hutumika kuipa nguvu busara ya kiongozi.

Tuseme meneja anaamini bidhaa fulani ndiyo inayopendwa zaidi na wateja. Badala ya kutegemea hisia hiyo, anaweza kuangalia mauzo ya miezi sita, maeneo yenye mahitaji makubwa, malalamiko ya wateja na faida inayopatikana.

Huenda data ikathibitisha alichokuwa anakiamini.

Lakini pia inaweza kumuonyesha alikuwa amekosea.

Hiyo ndiyo thamani yake: data inaweza kupima mawazo yetu kabla hayajageuka kuwa maamuzi ya gharama kubwa.

Uongozi unaotegemea data unaweza kusaidia kubaini matatizo, kutumia rasilimali vizuri, kufuatilia maendeleo, kuona hatari mapema na kutambua fursa zinazojitokeza.

## Anza na swali, si na namba

Makosa mengine hufanyika pale taasisi inapokusanya taarifa nyingi bila kujua inazitaka kwa sababu gani.

Kuwa na data nyingi hakumaanishi moja kwa moja kuwa una maarifa mengi.

Kiongozi anapaswa kuanza na swali.

Kwa mfano: Kwa nini mauzo yamepungua? Kwa nini wanafunzi wengi wanafeli somo fulani? Kwa nini wateja wanaondoka? Ni huduma ipi inatumia fedha nyingi lakini inaleta matokeo madogo?

Baada ya swali ndipo unatafuta taarifa zinazoweza kulijibu.

Hatua muhimu ni kuweka malengo, kutambua vyanzo vya taarifa, kukusanya data, kuichambua, kufanya uamuzi na baadaye kupima kama uamuzi huo umeleta matokeo yaliyotarajiwa.

Hivyo, data si mwisho wa safari. Ni sehemu ya mchakato wa kufanya uamuzi.

## Kiongozi lazima ajue kusoma data

Hapa kuna changamoto nyingine.

Si lazima kila mkuu wa taasisi awe mtaalamu wa takwimu, programu au sayansi ya data.

Lakini kiongozi wa sasa anahitaji uelewa wa data.

Anapaswa kuweza kuuliza: Taarifa hii imetoka wapi? Imekusanywa kwa watu wangapi? Inaonyesha nini? Haionyeshi nini? Je, kuna jambo muhimu tumeliacha? Je, tunaweza kufanya uamuzi mkubwa kwa ushahidi huu?

Hili ni muhimu kwa sababu data mbovu inaweza kuzaa uamuzi mbovu.

Taarifa isiyo kamili, iliyokusanywa vibaya au iliyotafsiriwa vibaya inaweza kuonekana ya kisayansi lakini bado ikampotosha kiongozi.

Ndiyo maana ubora wa data, uwazi wa vyanzo na uwezo wa kuitafsiri ni muhimu sawa na kuwa nayo.

## Data inaweza kuboresha matumizi ya rasilimali

Kila taasisi ina rasilimali zenye mipaka.

Fedha hazitoshi kila kitu. Wafanyakazi hawatoshi kila mahali. Muda nao una mwisho.

Data inaweza kusaidia kujua eneo gani lipewe kipaumbele.

Katika shule, kwa mfano, taarifa za mahudhurio na ufaulu zinaweza kusaidia kubaini kundi la wanafunzi linalohitaji msaada zaidi. Katika biashara, taarifa za mauzo zinaweza kuonyesha bidhaa inayokwenda vizuri, eneo lenye wateja wengi au kampeni ya matangazo isiyoleta matokeo. Katika taasisi, data inaweza kuonyesha mradi unaotumia fedha nyingi lakini haukidhi malengo.

Hapo uamuzi unahamia kutoka "nadhani" kwenda "ushahidi unaonyesha."

## Lakini data si kila kitu


Hata hivyo, kuna hatari ya kwenda upande mwingine na kuamini kwamba kila jambo linaweza kuamuliwa na jedwali au chati. Haiwezekani. Data inaweza kukuonyesha mfanyakazi amekosa kazi mara nyingi. Lakini inaweza isikuambie moja kwa moja kwamba anamhudumia mzazi mgonjwa nyumbani.

Inaweza kukuonyesha mauzo yamepungua. Haiwezi peke yake kueleza kila mabadiliko ya hisia za wateja.

Masuala ya maadili, motisha, utamaduni wa taasisi, utu na mazingira ya mtu hayawezi kila mara kubanwa kwenye namba.

Ndiyo maana uongozi bora unachanganya ushahidi na busara ya kibinadamu.

Kiongozi anauliza data inasema nini, lakini pia anauliza: Je, hali halisi inasema nini?



NA JUNAYNAT ALLY DAMA
0789 201 383

# Msaidie mtoto mwenye ulemavu, lakini usimnyime nafasi ya kukua

**MALEZI ya mtoto mwenye ulemavu au mahitaji maalumu yanaweza kuwa na changamoto nyingi. Mtoto anaweza kuhitaji msaada zaidi katika mawasiliano, kujifunza, kutembea, kula, kujihudumia au kuhusiana na watu wengine.**
**Kwa sababu hayo ni malezi yenye mahitaji ya ziada, wazazi wanaweza pia kufanya makosa kwa nia njema kabisa.**
**Mojawapo ni kumlinda mtoto kupita kiasi. Mzazi anaweza kusema: "Yeye hawezi." Hivyo anamlisha hata anapoweza kujifunza kula mwenyewe, anamvalisha kila siku, hamruhusu kufanya kazi ndogo nyumbani au humzuia kutoka nje kwa kuhofia ataanguka, atachekwa au atapata shida.**
**Lakini msaada usipowekwa katika kiwango sahihi unaweza kugeuka kuwa kizuizi. Lengo la malezi halipaswi kuwa tu kumkinga mtoto dhidi ya kila tatizo. Linapaswa pia kuwa kumsaidia kupata uwezo mkubwa zaidi wa kujitegemea kadiri hali yake inavyoruhusu.**

## Muone mtoto kwanza, si ulemavu

Hili ndilo jambo la kwanza muhimu.

Mtoto mwenye ulemavu bado ni mtoto.

Ana hisia. Ana hamu ya kucheza. Anaweza kuwa na vitu anavyovipenda na asivyovipenda. Ana uwezo fulani na udhaifu fulani.

Ndiyo maana wataalamu wanashauri wazazi na walezi wasitazame jina la ulemavu pekee, bali waangalie mahitaji halisi ya mtoto mmoja mmoja. Watoto wawili wenye utambuzi unaofanana wanaweza kuwa na uwezo na changamoto tofauti kabisa. Usimfanye mtoto maisha yake yote kuwa "matibabu."

Kuna wakati wa tiba, mazoezi na mafunzo. Lakini pia kuna wakati wa kucheza, kucheka, kutoka nje, kushiriki na familia na kuwa mtoto wa kawaida.

## Usimfanyie kila kitu

Mtoto mwenye ulemavu anaweza kuhitaji msaada, lakini hiyo haimaanishi hawezi kufanya chochote.

Mpe kazi ndogo kulingana na uwezo wake. Anaweza kuweka kikombe mezani. Anaweza kusaidia kupanga nguo. Anaweza kujifunza kupiga mswaki, kuvaa sehemu ya nguo mwenyewe au kuleta kitu kutoka chumba kingine.

Anapojaribu kufanya jambo, usikimbilie kulifanya kwa niaba yake kwa sababu tu analifanya polepole. Mpe muda. Msaidie pale anapohitaji msaada.

Lengo si mtoto kufanya kila kitu kama watoto wengine. Lengo ni kufikia kiwango cha juu zaidi cha uwezo wake mwenyewe. Njia hii humjengea kujiamini na hisia kwamba yeye pia anaweza kufanya mambo yenye maana.

## Mruhusu kufanya maamuzi

Watoto wenye ulemavu wakati mwingine hujikuta watu wazima ndio wanaamua kila kitu kwa niaba yao.

Atavaa nini. Atakula nini. Atakaa wapi. Ataenda wapi. Lakini mtoto pia anahitaji kujifunza kuchagua.

Anza na mambo madogo: "Unataka shati jekundu au la bluu?" "Unataka embe au ndizi?" "Tuanze kusoma au kucheza?"

Kumpa uchaguzi unaolingana na uwezo wake humfundisha kufikiri, kufanya maamuzi na kuelewa kwamba maoni yake yana thamani.

Katika mazingira ya malezi na elimu, mtoto anapaswa kupewa nafasi ya kuchagua, kujaribu na kupata furaha ya kufanikisha jambo mwenyewe

## Usimfiche nyumbani

Baadhi ya wazazi huwazuia watoto wenye ulemavu kushiriki kwenye shughuli za familia kwa hofu ya kuangaliwa, kuulizwa maswali au mtoto kufanya jambo litakalovuta macho ya watu.

Lakini kumfungia mtoto nyumbani hakumalizi tatizo. Kunamnyima nafasi ya kujifunza namna ya kuishi na watu.

Mpeleke kwenye shughuli za familia inapowezekana. Mruhusu kucheza na watoto wengine. Mshirikishe kwenye matembezi, sherehe na mazingira mbalimbali kulingana na hali yake na usalama wake.

Ushirikishwaji ni muhimu kwa sababu mtoto hujifunza kutokana na kukutana na watoto wengine na mazingira yanayomzunguka. Pia hujenga hali ya kujiamini na kujihisi sehemu ya jamii.

## Sherehekea maendeleo, usimlinganishe

Mtoto wako anaweza kuchelewa kusema. Anaweza kuchukua muda kujifunza kutembea, kuvaa au kufanya jambo ambalo watoto wengine hufanya kwa urahisi.

Usitumie maendeleo ya mtoto mwingine kama kipimo pekee cha maendeleo yake.

Kitu ambacho kwa mtoto mwingine ni kawaida kinaweza kuwa mafanikio makubwa kwa mtoto wako.

Alitamka neno jipya? Ameweza kula mwenyewe? Amejaribu kuzungumza na mtoto mwingine? Amekamilisha kazi aliyoshindwa mwezi uliopita? Litambue hilo.

Kusifu maendeleo ya kweli humsaidia mtoto kujenga kujiamini na hamasa ya kuendelea kujaribu.

## Mzazi naye anahitaji msaada

Malezi haya yanaweza kuchosha kimwili na kihisia.

Mzazi anaweza kuwa na miadi mingi hospitalini, gharama za matibabu, maswali kuhusu shule, hofu ya maisha ya baadaye na wakati mwingine kukabiliana na mitazamo mibaya ya jamii.

Usijione lazima ubebe kila kitu peke yako.

Shirikiana na mwenzi wako, ndugu, walimu, wataalamu wa afya na wazazi wengine wanaopitia hali zinazofanana.

Mzazi anamjua mtoto kwa namna ambayo mtaalamu hawezi kumjua, na mtaalamu ana maarifa ambayo mzazi anaweza kuyahitaji. Ushirikiano huo ndio huleta matokeo bora zaidi.

Malezi ya mtoto mwenye ulemavu hayahitaji huruma pekee. Yanahitaji upendo wenye busara.

Msaidie pale anapohitaji msaada, lakini usimnyime nafasi ya kujaribu. Mlinde anapohitaji ulinzi, lakini usimzuie kuiona dunia.

Kwa sababu mwisho wa yote, lengo si tu kumtunza mtoto leo.

Na Samrath Msuya
0789 201 383

# Ubunifu katika ufundishaji hisabati

## SEHEMU YA 1

## Kwa nini watoto wengi huiogopa hesabu? Huenda tatizo si hesabu yenyewe

**Kwa watoto wengi, kutajwa tu kwa neno "hisabati" kunatosha kuleta hofu. Wengine hukaa kimya darasani wakihofia kuitwa ubaoni. Wengine huingia kwenye mtihani wakiwa tayari wamekata tamaa wakiamini kwamba wao "si watu wa hesabu", kana kwamba uwezo wa kuelewa somo hilo ni kipaji ambacho mtu huzaliwa nacho au hukikosa kabisa. Kwa mujibu wa gazeti la Mwananchi, mwaka 2025 asilimia 43.3 ya wanafunzi walipata wastani wa alama D na F, ikilinganishwa na asilimia 44.9 mwaka 2024. Hata hivyo, kati ya mwaka 2020 na 2022 zaidi ya nusu ya wanafunzi walifaulu kwa kupata alama A, B na C.**
**Takwimu zinatufanya tujiulize, Kwa nini somo linalotumika karibu kila sehemu ya maisha linaendelea kuwa gumu kwa wanafunzi wengi? Je, tatizo ni uwezo wa watoto au udhaifu katika ufundishaji?**

### Hesabu si kukariri kanuni pekee

Wengi wetu tulijifunza hesabu kwa mfumo unaofanana: mwalimu anaonyesha namna ya kutatua swali, wanafunzi wanafuata hatua hizo, kisha wanapewa maswali mengine yanayofanana. Aliyekumbuka utaratibu na kanuni vizuri ana nafasi kubwa ya kupata jibu sahihi.

Njia hiyo ina nafasi yake. Mtoto lazima ajifunze kujumlisha, kutoa, kuzidisha, kugawanya na kutumia kanuni mbalimbali za hisabati. Lakini kujua kanuni si mwisho wa kujifunza hesabu. Mwanafunzi anahitaji pia kuelewa anachofanya, kwa nini anakifanya na lini maarifa hayo yanaweza kutumika.

Katika maisha halisi, matatizo hayaji yakiwa yameandikwa chini yake: "Tumia kanuni hii." Tunatumia hesabu kupanga matumizi ya fedha, kufanya biashara, kupima, kujenga, kulinganisha bei, kupanga safari, kusoma takwimu na kufanya maamuzi mbalimbali. Haya yanahitaji zaidi ya uwezo wa kukumbuka kanuni; yanahitaji uwezo wa kufikiri na kutatua tatizo.

Wataalamu wa elimu ya hesabu wanaeleza ubunifu wa kihesabu kuwa pamoja na uwezo wa kuona njia tofauti za kutatua tatizo, kubadili njia pale moja inaposhindikana, kutoa mawazo mbalimbali na kueleza kwa nini njia au jibu fulani lina mantiki.

### Jibu sahihi ni muhimu, lakini si kila kitu

Mtoto anaweza kukariri hatua za kutatua aina fulani ya swali na kupata jibu sahihi kila anapokutana na swali linalofanana. Lakini swali likibadilishwa kidogo, akashindwa kabisa. Katika hali hiyo, huenda hajui hesabu kwa kina; anachokijua ni kufuata utaratibu aliouonyeshwa.

Ndiyo maana katika ufundishaji wa kisasa, mwanafunzi anahimizwa asiwe msikilizaji tu. Apewe nafasi ya kuuliza, kujaribu, kujadili na kueleza alivyofikia jibu. NRICH, mradi wa elimu ya hisabati unaohusishwa na Chuo Kikuu cha Cambridge, unasisitiza umuhimu wa kuwapa wanafunzi nafasi ya kuchunguza matatizo na kufikiri wenyewe badala ya kubaki watazamaji wa mwalimu anayefanya hesabu.

Kwa hiyo, badala ya kila mara kuuliza "Jibu ni nini?", wakati mwingine mwalimu anaweza kuongeza swali muhimu zaidi: "Umefikiaje jibu hilo?" Swali hilo linampa mwanafunzi nafasi ya kueleza fikra zake na mwalimu nafasi ya kuona kama kweli ameelewa.

### Mtoto asiogope kukosea

Hofu ya kufanya kosa nayo inaweza kumfanya mwanafunzi aione hesabu kama adhabu. Kama kila jibu lisilo sahihi linaishia kwenye aibu, kejeli au adhabu, mtoto mwenye mashaka anaweza kuamua kwamba njia salama zaidi ni kukaa kimya na kutojaribu.

Kosa linaweza kuwa sehemu muhimu ya safari ya kujifunza Mwalimu anaweza kulitumia kuuliza mwanafunzi alifikiria nini, alikosea wapi na angeweza kujaribu njia gani nyingine.

Hii haimaanishi kwamba jibu sahihi halina umuhimu. Lina umuhimu mkubwa. Lakini mtoto anayeelewa kwa nini jibu ni sahihi anajenga msingi bora zaidi kuliko yule anayejua tu kwamba akifuata hatua fulani atafika kwenye jibu.

### Si mwalimu pekee anayebeba mzigo

Haitakuwa sahihi kuhusisha changamoto ya ufaulu wa hesabu na mbinu za ufundishaji pekee. Madarasa yenye wanafunzi wengi, uhaba wa walimu na vifaa, mazingira ya shule, muda wa kujifunza, lugha ya kufundishia na msingi aliojengewa mtoto katika madarasa ya awali vinaweza pia kuwa na nafasi.

Hata hivyo, namna tunavyofundisha na kuzungumza kuhusu hesabu ni sehemu ambayo tunaweza kuanza kuibadilisha. Na si jukumu la mwalimu pekee. Mzazi anapomwambia mtoto, "Mimi mwenyewe nilikuwa sifahamu hesabu," huenda anataka kumfariji, lakini pia anamjengea fikra kwamba kutoweza hesabu ni hali ya kudumu.

### Tuione hesabu kwa jicho tofauti

Hisabati si mkusanyiko wa kanuni za kukariri ili kufaulu mtihani. Ni namna ya kufikiri, kuona uhusiano kati ya mambo, kuuliza maswali na kutafuta suluhisho. Kadiri tunavyowapa watoto nafasi ya kufikiri badala ya kufuata maelekezo pekee, ndivyo tunavyoweza kuwasaidia kuiona hesabu kama jambo wanaloweza kulielewa badala ya somo la kuliogopa.

Katika makala ijayo tutaangalia namna mwalimu anavyoweza kumsaidia mwanafunzi asiishie kutafuta jibu sahihi pekee, bali ajifunze kufikiri kihesabu.

ربيع أول



Na Junaynat Ally Dama

# Uandishi wa habari kwa msaada wa AI

SEHEMU YA 1

## AI imeingia chumba cha habari: Tuikatae au tujifunze kuitumia?

**Akili mnemba, maarufu kwa kifupi cha AI, imeingia kwa kasi katika maisha yetu. Inaandika, inatafsiri, inachambua taarifa, inatengeneza picha na inaweza kujibu maswali ndani ya sekunde chache.**

### Kwa mwandishi wa habari, AI inavutia sana.

Una mahojiano ya dakika 40 ya kunukuu? AI itayabadilisha kuwa maandishi. Una ripoti ya kurasa 200? Itabaini maeneo muhimu ya kuanzia. Itapendekeza maswali ya mahojiano, itashauri kichwa cha habari nk.

Kwa hiyo, AI ni sehemu ya mazingira ya kisasa ya kazi katika vyumba vya habari.

Lakini ikiwa AI inaweza kufanya mambo mengi hivi, mwandishi wa habari anabaki na kazi gani? Jibu ni rahisi: kazi zake zilezile.

### AI inasaidia lakini sio mwandishi wako

Uandishi wa habari si kupanga maneno mazuri pekee.

Mwandishi anatakiwa kutambua jambo lenye umuhimu kwa jamii, kukutana na watu, kuuliza maswali, kusikiliza, kutafuta nyaraka, kulinganisha madai, kuchunguza maslahi mbalimbali na hatimaye kuamua ni taarifa gani inaaminika na ipi haijaaminika.

Hapo ndipo tofauti kubwa kati ya mwandishi na AI ilipo. AI inaweza kukusaidia kutengeneza maswali 20 ya kumuuliza waziri. Lakini haiwezi kusoma uso wa waziri wakati anakwepa swali.

Inaweza kukusaidia kuchambua hotuba. Lakini haiwezi kwenda kijijini kuona kama ahadi iliyotolewa katika hotuba hiyo imetekelezwa.

Inaweza kupendekeza 'angle' ya habari. Lakini uamuzi kwamba angle hiyo ni ya haki, muhimu na yenye maslahi kwa umma unabaki kwa mwandishi na mhariri.

Kwa maneno mengine, AI inaweza kusaidia katika kazi ya uandishi wa habari, lakini haiwezi kubeba wajibu wa uandishi wa habari.

### Msaidizi mwenye kasi — lakini anayehitaji kusimamiwa

Tatizo la AI inajibu kwa kujiamini hata pale inapokosea.

Mifumo mingi ya AI haifanyi kazi kama maktaba inayotoa ukweli uliothibitishwa. Hutumia mifumo ya kitakwimu kutengeneza jibu linaloonekana kufaa kutokana na maelekezo na taarifa ilizonazo.

Hivyo, jibu linaloonekana zuri si lazima liwe sahihi. AI inaweza kukupa jina, tarehe, takwimu au rejea inayosikika kabisa kama ya kweli, lakini ukichunguza ukakuta haipo au si sahihi.

Kwa hiyo, mwandishi hapaswi kusema: "ChatGPT imesema, kwa hiyo ni kweli."

Kanuni sahihi ni: AI ikupe pa kuanzia; chanzo halisi kikupe ukweli wa kuchapisha. Ukipata takwimu, tafuta ripoti yake. Ukipata nukuu, tafuta mahali ilipotolewa. Ukipata madai kuhusu sheria, soma sheria au muulize mwenye mamlaka.

AI haiondoi kazi ya kuhakiki. Inaweza kufanya umuhimu wa kuhakiki uwe mkubwa zaidi.

### Inaweza kukuokoa muda

Hata hivyo, licha ya tahadhari hizo tusiikimbie AI. Ikitumiwa vizuri, inaondoa kazi zinazotumia muda mwingi na kumwachia mwandishi nafasi ya kufanya uandishi wa habari wenye thamani zaidi.

Fikiria mwandishi mwenye ripoti kubwa ya CAG. Anaweza kuiomba AI imsaidie kutambua maeneo yenye takwimu zinazojirudia, tofauti kubwa au masuala yanayohitaji uchunguzi zaidi.

Lakini hatua inayofuata bado ni yake: kusoma ukurasa husika, kuthibitisha takwimu, kutafuta wahusika na kufanya mahojiano.

Hapo AI haijamwondoa mwandishi. Imemwondolea baadhi ya kazi za kuchosha ili awe na muda zaidi wa kufanya kazi ya kiandishi.

### Hatari nyingine: Kuacha kufikiri

Mwandishi akizoea kila mara kuuliza AI: "Nipe angle," "niandikie ufunguzi," "nipangie maswali," "niandikie habari," anaweza taratibu kuacha kufanya baadhi ya mazoezi yanayojenga uwezo wake wa kitaaluma.

Uandishi hujifunzwa kwa kuandika. Maswali mazuri hujifunzwa kwa kufanya mahojiano. Angle nzuri hujengwa kwa kusoma, kufikiri, kukutana na watu na kuelewa jamii.

Hata katika zama za AI, mwandishi anahitaji kukaa na chanzo, kusikiliza kwa makini, kutembelea eneo la tukio na wakati mwingine kukaa mbele ya ukurasa mtupu akifikiri mwenyewe.

Teknolojia isitufanyie kazi kiasi cha kutufanya tushindwe kuifanya bila teknolojia.

### Mwandishi ndiye mwenye usukani

Historia ya uandishi wa habari imejaa teknolojia mpya.

Kulikuwa na mashine ya kuandika. Kinasa sauti kisha TV vikaja. Kompyuta ikaja. Intaneti ikaja. Simu janja na mitandao ya kijamii vikabadilisha tena namna tunavyotafuta na kusambaza habari.

AI ni hatua nyingine kubwa katika mabadiliko hayo ila tofauti yake ni kwamba inaweza kuonekana kana kwamba "inafikiria" pamoja nasi. Hilo ndilo linaloifanya kuwa na nguvu kubwa — na pia kuhitaji tahadhari kubwa.

Kanuni nzuri ya kuanzia ni hii: AI inaweza kupendekeza. Mwandishi ndiye anaamua. AI inaweza kuchambua. Mwandishi ndiye anahakiki. AI inaweza kusaidia kuandika. Mwandishi ndiye anayewajibika kwa kilichochapishwa.

### Jaribu hii kwa AI

Ukiwa na wazo la habari, badala ya kusema: "Niandikie habari kuhusu ongezeko la gharama za maisha." jaribu kusema: "Nisaidie kutengeneza orodha ya maswali 15 ambayo ninapaswa kuuliza. Gawa maswali katika sababu, athari kwa wananchi, takwimu muhimu, wahusika wa kuhoji na suluhisho. Usinitungie facts."

Hapo AI inakusaidia kujiandaa kufanya uandishi wa habari badala ya kukufanyia.

Na Junaynat Ally Dama

# Si masaa tu, ubora wa usingizi pia muhimu kwa afya



Watu wengi wanapozungumzia usingizi mzuri huanza na swali moja: Umeshinda saa ngapi ukilala? Lakini hiyo ni nusu tu ya picha.

Unaweza kuwa umelala saa saba au nane, lakini kama usingizi wako ulikuwa wa kukatika-katika, ulilala kwa shida, ulilala muda usio wa kawaida au uliamka ukiwa bado umechoka, huenda mwili wako haukupata mapumziko unayohitaji.

Kwa hiyo, afya ya usingizi haiwezi kupimwa kwa kuhesabu masaa pekee. Ubora wa usingizi ni muhimu karibu sawa na muda tunaotumia kulala.

Makala moja katika tovuti ya American Heart Association inaeleza kuwa afya ya usingizi inahusisha vipengele mbalimbali ikiwemo muda unaochukua kupata usingizi, kuendelea kulala bila kuamka mara kwa mara, muda wa kwenda kulala, kuwa na ratiba inayofanana kila siku na jinsi mtu anavyojisikia baada ya kuamka.

## Saa saba au tisa hazitoshi peke yake

Kwa watu wazima, kwa ujumla, saa saba hadi tisa za usingizi kwa usiku hupendekezwa. Hata hivyo, mahitaji hutofautiana kati ya mtu na mtu kutokana na umri, afya na hali nyingine binafsi.

Tatizo linakuja pale tunapochukulia muda huo kama kipimo pekee cha afya ya usingizi.

Fikiria mtu amelala saa nane lakini akaamka mara sita usiku. Mwingine amelala saa nane lakini amechukua zaidi ya saa moja kupata usingizi. Kwa hesabu, wote wanaweza kusema "nimelala saa nane." Lakini kwa ubora wa usingizi, hali zao zinaweza kuwa tofauti sana.

Ndiyo maana wataalamu huangalia pia kama usingizi unaendelea vizuri bila kuvurugika na kama mtu anaamka akiwa amepumzika.

## Usingizi una hatua tofauti

Usingizi si hali moja inayodumu usiku mzima. Mwili hupitia hatua mbalimbali za usingizi, zikiwamo hatua za usingizi mwepesi, usingizi mzito na hatua inayojulikana kama REM, ambayo ndoto nyingi hutokea.

Hatua ya usingizi mzito ni muhimu katika kurejesha mwili na kusaidia mfumo wa kinga. Cleveland Clinic inaeleza kuwa mtu asipopata usingizi mzito wa kutosha anaweza kuamka akiwa amechoka hata kama amekaa kitandani kwa muda mrefu.

## Ratiba nayo ina maana

Ubora wa usingizi unahusiana pia na muda tunaolala.

Kulala saa tofauti sana kila siku kunaweza kuvuruga saa ya ndani ya mwili, inayojulikana kitaalamu kama circadian rhythm. Huu ni mfumo wa asili unaosaidia mwili kujua wakati wa kuwa macho na wakati wa kupumzika.

Ndiyo maana kuwa na muda unaokaribiana wa kulala na kuamka kila siku kunaweza kusaidia. Ushahidi unaonyesha kuwa uthabiti wa ratiba ya usingizi ni sehemu muhimu ya afya ya usingizi.

Kwa maneno mengine, si jambo zuri sana kulala saa nne leo, saa 10 kesho na saa sita siku inayofuata halafu kutegemea kwamba wastani wa masaa utakutatulia kila kitu.

Mwili unapenda utaratibu.

## Usingizi mbovu unaweza kuathiri moyo

Sababu ya kulipa suala hili uzito ni kwamba usingizi hauhusiani na uchovu pekee.

American Heart Association imeeleza kuwa usingizi usioridhisha umehusishwa na matatizo mbalimbali yanayoweza kuongeza hatari ya magonjwa ya moyo na mishipa ikiwemo shinikizo la juu la damu, sukari katika damu, unene kupita kiasi na baadhi ya matatizo ya moyo.

UKHTI FATIMA SS

# Maswali 10 ya kumjua mtu kwa undani

**WAKATI mwingine unaweza kuwa umemfahamu mtu kwa miaka mingi lakini bado usijue mengi kuhusu dunia yake ya ndani.**

**Unajua anafanya kazi wapi, anapenda chakula gani, anatoka wapi na labda hata marafiki zake. Lakini hujui kitu gani kinamuumiza zaidi, anaogopa nini, anataka kukumbukwa kwa jambo gani au ni tukio gani lililombadilisha kabisa.**

**Nilikutana na nukta hizi katika klipu iliyowekwa mtandaoni na mwandishi wa habari Frank Mavura, nikaona zinafaa kushirikishwa kwa sababu zinaweza kusaidia kufungua mazungumzo ya kina zaidi.**

**Kisaikolojia, maswali mazuri yanaweza kutusaidia kuelewa hisia, maadili, hofu, matarajio na uzoefu uliomjenga mtu.**

## Haya ni maswali 10 ya kujaribu.

**Ni jambo gani ambalo watu wengi hawalijui kuhusu wewe?**

Hili humtoa mtu kwenye maelezo ya kawaida anayowaambia kila mtu.

Jibu linaweza kufichua kipaji, tukio, hisia, mapambano au sehemu ya maisha yake ambayo kwa kawaida haionyeshi.

Ni swali linaloweza kukupeleka kutoka "ninamjua" kwenda "ninaanza kumwelewa."

**Ni kitu gani kinachokufanya ujisikie unapendwa na kuthaminiwa?**

Watu hawapokei upendo kwa namna moja.

Mmoja anathamini maneno ya kutambua juhudi zake. Mwingine anathamini muda wa pamoja. Mwingine msaada, uaminifu au vitendo vidogo vya kujali.

Jibu lake linaweza kukuonyesha mahitaji yake ya kihisia na mambo anayoyatafsiri kama ishara ya kujaliwa.

**Ni tukio gani katika maisha lililokubadilisha zaidi?**

Watu wengi wameumbwa na matukio ambayo hayaonekani kwa macho.

Inaweza kuwa kufiwa, kushindwa, kupata mtoto, kufanikiwa, kuugua, kuhamia sehemu mpya au kukutana na mtu aliyebadili mwelekeo wa maisha.

Swali hili linasaidia kuelewa uzoefu uliomjenga na mafunzo aliyobeba hadi leo.

**Ni jambo gani unaloliogopa zaidi maishani?**

Hofu inaeleza mengi kuhusu mtu.

Mmoja anaogopa kushindwa. Mwingine kuachwa. Mwingine kuzeeka bila kutimiza ndoto zake. Mwingine kupoteza familia, afya au heshima.

Hofu inaweza kufichua udhaifu, lakini pia kile mtu anachothamini sana.

Mara nyingi tunaogopa kupoteza kitu chenye maana kubwa kwetu.

**Unapokuwa na tatizo, unapenda kusaidiwa au kupewa nafasi yako mwenyewe?**

Hili ni swali muhimu sana katika mahusiano.

Kuna watu wanapopitia shida wanahitaji mtu awe karibu nao. Wengine wanahitaji muda wa kuwa peke yao kwanza, wafikiri na kutulia.

Kutokujua tofauti hii kunaweza kuzaa migogoro. Unaweza kudhani unamsaidia mtu kwa kumfuatilia sana, wakati yeye anahitaji nafasi.

Jibu linakuonyesha namna anavyoshughulikia msongo na changamoto.

**Ni kitu gani ambacho huwezi kuvumilia kwa mtu mwingine?**

Majibu hapa yanaweza kufichua mipaka na maadili.

Anaweza kusema uongo, usaliti, dharau, ubinafsi, ukatili au kutowajibika.

Kitu kinachomkera sana mtu mara nyingi kinahusiana na kile anachokiona kuwa muhimu katika mahusiano yake.

Hata hivyo, ni vizuri kusikiliza bila kukimbilia kumhukumu.

**Ni ndoto gani ambayo bado hujaitimiza?**

Hapa unaanza kumjua mtu kupitia kesho yake, si jana yake pekee.

Anaweza kuwa na ndoto ya kusoma zaidi, kujenga biashara, kusafiri, kuandika kitabu, kulea familia vizuri au kufanya kazi yenye maana kwake.

Ndoto zisizotimizwa zinaonyesha matarajio na mwelekeo ambao mtu bado anatamani kufuata.

**Ni kosa gani kubwa ulilowahi kufanya, na ulijifunza nini?**

Sio kila mtu atakuwa tayari kujibu hili mara moja.

Lakini jibu lake linaweza kuonyesha kiwango cha kujitambua na uwajibikaji.

Mtu anayekubali kosa lake na kueleza alichojifunza anaonyesha kitu tofauti na mtu anayesimulia kosa lakini anaishia kuwalaumu wengine wote.

Kosa lenyewe si jambo pekee muhimu. Muhimu zaidi ni namna mtu anavyolitazama leo.

**Unataka watu wakukumbuke kwa jambo gani?**

Hili linagusa kile wanasaikolojia na wanafalsafa wengi wamekuwa wakikiita maana au kusudi la maisha.

Je, anataka kukumbukwa kwa utajiri? Ukarimu? Uadilifu? Malezi? Uongozi? Elimu? Huduma kwa watu?

Jibu linaweza kufichua aina ya maisha anayotaka kuyaishi na urithi anaotaka kuuacha.

**Ni ushauri gani ungeutoa kwa wewe wa miaka iliyopita?**

Hili ni swali lenye nguvu kwa sababu linamlazimisha mtu kutazama safari yake kutoka nyuma.

Anaweza kusema: "Usiogope sana." "Anza mapema." "Usiwaamini watu kirahisi." "Tumia muda zaidi na wazazi wako." "Jifunze kusema hapana."

Ndani ya jibu hilo unaweza kukuta majuto, mafunzo na hekima aliyokusanya.

Lakini kuna tahadhari moja muhimu.

Maswali haya si dodoso la kumhoji mtu. Usiyapige yote kwa dakika 20 kama polisi.

Mazungumzo ya kina yanahitaji mazingira salama, muda na uaminifu. Mtu pia ana haki ya kutokujibu swali ambalo hayuko tayari kulijibu.